# CHUO CHA BIBLIA

# VITABU VYA
# ISAYA, YEREMIA, MAOMBOLEZO, EZEKIELI NA DANIELI

## KITABU CHA NANE

## SURA YA KWANZA

### ‘Tabia Ya Utu Wake Nabii’

Vitabu vya unabii vinafahamika kama kina kikuu cha Agano la Kale, hasa kutokana na mtazamo wa Agano Jipya. Katika kazi ya ujenzi wa Kanisa ya Kristo aliyefufuka hadi itakapoondolewa. Sheria ni vitabu vitano vya Kwanza vya Biblia - Mwanzo, Kutoka, Walawi, Hesabu, na Kumbukumbu la Torati. Nao Manabii ni vile vitabu ambavyo sasa tunaiandaa kusoma, tukianzia na Isaya na kumalizia na Malaki.

Kuna mtazamo uliopo katika vitabu vya manabii ambao unadhihirishwa na mtume Paulo wakati alipokuwa na mazungumzo na mfalme. Mtume alikuwa kwenye minyororo huku akitangaza Injili kwa uwezo mkuu, hivi kwamba hata yule mfalme akasema kwamba Paulo alikuwa yu karibu kumshawishi kufanyika mwaminifu wa Kristo. Tukio kuu katika ushuhuda wa mtume Paulo ulikuwa wakati alipomwuliza swali hili, *‘Mfalme Agripa, Je! Wewe waamini hao manabii?* Mimi nafahamu kwamba wewe waamini hao manabii!’ Swali hili la Paulo liliulizwa wakati mwingine kuhusu hao manabii. Mahubiri yao pamoja na Maandiko yalikuwa yamevuviwa wala sio ya kawaida, na njia moja ya kutambua mtu ikiwa ni mwanamume au mwanamke wa imani ilikuwa ni kuuliza swali, *‘Je! Unaamini hao manabii?’*

Wakati Agano Jipya linapowataja manabii, huwa linawataja wale ambao waliandika vitabu vya unabii, au nakala ya vitabu vya unabii. Kuna vitabu kumi na saba vya unabii vilivyoandikwa na yamkini manabii kumi na sita. (Yeremia aliandika vitabu viwili - Yeremia na Maombelezo)’

Kabla ya kuanza uchunguzi wetu wa vitabu hivi vya manabii, ningependa kujibu swali hili, ‘Kwa hakika nani ndio manabii?’ Nitalianza jibu kwa swali hilo kwa kuwalinganisha manabii na

makuhani. Wakati vitabu vya sheria vilipoandikwa, aliyekuwa kiongozi mwenye umuhimu alikuwa Kuhani. Kuhani alikuwa na wajibu muhimu sana kwa kuwa alikuwa mwombezi wa watu wakati wanapotenda dhambi. Pia wao walifafanua na kueleza Maandiko kwa watu wake Mungu. Makuhani walikuwa walimu wa watu wa Mungu. Wao walijibu maswali kuhusu Maandiko, dhabihu na desturi katika Hema la Ibada huko nyikani, na baadaye katika Hekalu la Sulemani.

Kuhani alizaliwa akiwa kuhani kwa kuwa alikuwa mzaliwa wa kizazi cha Haruni au Lawi. Na kwa nusra mbovu, wakati mwingi hao makuhani walifanyika kuwa watu fisadi na watenda maovu. Hosea alibuni msemo huu, *'Jinsi walivyo makuhani ndivyo, walivyo watu.'* Wakati mwingi, watu walipofanyika kuwa waasi na wenye dhambi, ni hao makuhani walifanyika viongozi katika njia potovu. Na wakati makuhani walipofanyika kuwa wafisadi na wenye dhambi, Mungu aliwatuma manabii.

Manabii hawakuzaliwa wakiwa hivyo. Hawa ni watu ambao walipata mwito wake Mungu kutoka tabaka mbali mbali. Yamkini wawili au watatu miongoni mwao walikuwa makuhani walipoupokea mwito wa kuwa manabii, lakini hii haikuwa jambo la kawaida. Miongoni mwa manabii walikuwemo wazaliwa kutoka mbari na nyumba za kifalme, ilhali wengine walipokea mwito wao wakiwa watu kutoka hali mbali mbali za maisha kama Amosi, ambaye alikuwa mchuna mibuyu na mchungaji wa mifugo. Kwa uhakika, kuhani alikuwa mtu ambaye alikwenda mbele katika uwepo wa Mungu na kufanya maombi kwa Mungu kwa niaba ya watu wengine. Naye nabii alikuwa mtu ambaye alitoka katika uwepo wa Mungu na kuwaeleza watu mausia na ujumbe kutoka kwa Mungu.

Manabii wale ambao waliandika vitabu waliishi katika kipindi cha miaka mia nne, tokea mwaka wa 800 Kabla ya kuzaliwa kwake Kristo hadi mwaka wa 400 Kabla ya kuzaliwa kwake Kristo. Katika nyakati hizo, watu walikuwa wamejitosa katika dhambi, hasa dhambi ya kuabudu sanamu. Kwa kuwa walikuwa waabudu wa miungu mingine, hukumu yake Mungu ilikuwa ikikaribia juu yao kwa mfano nchi ya Ashuru kuwavamia na kuwachukua mateka ufalme wa kaskazini. Hii ilifuatiwa baadaye yapata miaka mia moja na uvamizi kutoka huko Babeli ulipowafanya wale kutoka ufalme wa kusini kuchukuliwa mateka. Baadhi ya manabii waandishi wa vitabu hivi walitangulia kutekwa huku na wengine walihusika kwenye utekaji nyara huo na kuhudumu kwa miaka utumwani, walipata kuishi nyakati za kurudi kwao kutoka utumwani, au wengine walipata kuishi miongoni mwa matukio haya yote.

Miongoni mwa manabii waandishi kumi na sita, watatu wao walihudumu na kuhubiri baada ya kutekwa huko na mahubiri yao yalizungumzia kuhusu ujenzi upya na kuhuishwa kuliofuatia kurejeshwa kwa watu wa Mungu kutoka utumwani huko Babeli. Hata hivyo, wengi wao walitangulia kule kuvamiwa kwa ufalme ya Israeli wa kaskazini na wa kusini, au yamkini walitangulia matukio haya ya uvamizi na utekaji nyara, au hata walihudumu nyakati hizo.

Manabii waliotangulia utekaji nyara wa Waashuru dhidi ya ufalme wa kaskazini, na utekaji nyara kutoka kwa taifa Wababeli, ujumbe wao mkuu ulikuwa: *'Ikiwa mtakuwa na ufufuo wa kiroho, na ikiwa mtayaghairi na kutubu matendo ya dhambi zenu ya kuabudu sanamu, utumwa wenu huko Ashuru au Babeli hautatukia.'* Hawa manabii walitoa mwito wa toba na uamsho wa kiroho. Hata hivyo wakati mwingi, ujumbe wao haukutiliwa maanani, bali ulipuuziwa tu. Manabii hawa walidhihakiwa, na kutaniwa, na wakati mwingi waliteswa na kuuawa. Wengi wao walikufa kwa kuwa waliuhubiri ujumbe ambao hakuna aliyetaka kusikia.

Wakati manabii walipotambua kwamba watu hawakuwa wakisikia ujumbe wao, walianza kuhubiri kwamba, *'kutekwa nyara kwaja, na wakati kujapo, kutakuwa ni hukumu kutoka kwake Mwenyezi Mungu juu yenu, kwa kuwa mmekataa kutubu dhambi yenu ya ibada ya sanamu.'* Wao walikuwa wakisema ukweli. Wakati wana wa Ashuru walipoteka ufalme wa kaskazini, wao hawajawahi kusikika tena. Baadaye, Wababeli walivamia ufalme wa kusini, yaani Yuda.

Manabii walihubiri ujumbe wa tumaini kuhusu uvamizi wa Babeli.Walipokea ufunuo wa unabii na kuhubiri hivi: *'Miaka sabini baada ya utumwa wenu huko Babeli, mtarudi nyumbani.'* Wao waliona kurudi kwao kutoka utumwani huko Babeli kama kuwa ni dhihirisho la rehema na neema yake Mungu. Wengi wa hawa manabii hawakupata kuishi hadi kushuhudia muijiza huu.

**Unabii Wa Kimasihi**

Funzo lingine kuu la ujumbe wa manabii ni kuhubiri kuhusu kutawanyika kwa watu wa Mungu katika miisho ya ulimwengu. Wakati walipohubiri kuhusu kutawanyika kwa wana wa Israeli, pia walikuwa wakitabiri kuhusu kurudi kutoka utumwani huko Babeli. Wao walichanganya unabii wa Masihi na ule wa kurudi kwao kutoka utumwani.

Manabii walitangaza kuja kwake Kristo kwa mijio miwili. Atakuja mara ya kwanza kama Mwokozi aliyedhihakiwa na kuteseka na hatimaye kufa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu, lakini atakapokuja kwa mara ya pili, - sisi waaminifu tunataja mjio huu kama kuja kwa mara ya pili kwake Yesu Kristo. Yeye atakuja kwa mara ya pili kama Mfalme wa wafalme na Bwana wa Mabwana kushinda nguvu za muovu na kuazisha mbingu na nchi mpya ambapo haki ndiyo itatawala daima.

Wakati mwingi ni vigumu kutofautisha kati ya unabii wa Kimasihi na ule wa kurudi kutoka utumwa wa Babeli. Ni vigumu pia kutofautisha kati ya unabii wa kuja kwake Kristo kwa mara ya kwanza na kwa mara ya pili na unabii unaotufikia siku ya leo. Unabii wa Kimasihi kuhusu mijio hiyo miwili ya Yesu Kristo ni wa kusisimua sana katika vitabu hivi vya unabii.

**Wanenaji Wake Mungu**

Wakati tunaposikia neno 'Nabii', huwa tunafikiria wajibu wa nabii kama ule wa 'mtabiri wa hali ya hewa wa kiroho' , ambaye anaweza kutueleza habari za hali ya hewa ya hapo kesho. Neno 'Nabii' maanayake sahihi ni 'Yule anenaye kwa niaba ya Mungu.' Hivyo basi, nabii alikuwa mwanadamu ambaye Mungu alizungumza kumpitia kwake. Manabii hawa walinena kwa njia mbili. Kwanza kabisa, 'walitangaza' neno la Mungu, maanake kwamba walikuwa wahubiri wakuu wa Biblia. Pili 'walinena yatakayotokea', au walitabiri matukio yaliokuwa bado hayajatokea. Baadhi ya matukio waliyotabiri bado hayajatokea.

Sisi huvutiwa sana na eneo la kutabiri mambo yajayo katika huduma ya nabii. Ilikuwa ni sehemu yenye uwezo mkuu ya huduma yake nabii, lakini pia ilikuwa ni sehemu ndogo sana. Manabii walikuwa wahubiri. Wao walihimiza watu kulitii Neno la Mungu na kulitimiza katika maisha yao. Manabii walipokea ufunuo kuhusu kweli mpya, lakini wakati mwingi kuanzia wakati wa Yoshua, wao walihubiri Neno lililoandikwa na kutolewa kupitia Musa. Hii ndiyo sababu tunamtaja nabii Musa kuwa jitu miongoni mwa manabii wengi kwa kuwa alipokea Neno lake Mungu, ambalo manabii wengine walitumia katika mahubiri yao.

Neno 'Nabii' katika lugha ya Kiyunani ni muunganisho wa maneno mawili ambayo maana yake ni 'kusimama mbele ya' na 'kutia nuru.' Nabii alisimama mbele ya Neno la Mungu lililoandikwa na kulitia nuru, au kulifanya kuwa na mwanga. Pia aliwahimiza watu wa Mungu kutii na kutimiza neno Lake katika maisha yao. Wakati alipopokea ufunuo kuhusu mambo yajayo, yule nabii wakati wote aliwahimiza watu wa Mungu kuishi maisha ya utakatifu kulingana na nuru Mungu aliyompa ili kushiriki nao kuhusu mambo hayo.

**Hakuna Shida, Hakuna Nabii**

Nabii alitokea tu wakati kulipokuwa na matatizo. Hivyo tunaweza kusema kwamba, 'hakuna nabii, ikiwa hakuna shida.' Utakapokuwa ukijifunza kuhusu hawa manabii, unahitajika kuuliza maswali kama haya, 'Ni shida gani ambayo ilikuwa kikwazo kwa kazi ya Mungu wakati mtu fulani alipotokea na mwito wa nabii, na ni jinsi gani huduma yake ilisaidia katika kuondoa vikwazo vilivyokuwa vikizuia kazi ya Mungu siku ile?'

Kwa mfano, katika nyakati za nabii Hagai, ambazo ni kurudi kutoka utumwani huko Babeli, kazi yake Mungu ilikuwa kuhusu ujenzi wa Hekalu huko Yerusalemu. Wakati wana wa

Mungu walipoanza ujenzi wa Hekalu kwa mara ya pili, iliwabidi kuvumilia majaribu makuu. Ingawa mfalme wa Uajemi (Persia) alikuwa amewapa ruhusa kurudi na kuwapa baadhi ya vyombo vya ujenzi wa Hekalu, wao walikumbana na pingamizi wakati walipoanza ujenzi wao.

Wakati dhiki ilipoanza, waliacha kutenda kazi ya ujenzi wa Hekalu. Waliacha nia hiyo na kujitosa katika ujenzi wa nyumba zao wenyewe. Waliendelea kufanya hivyo kwa muda wa miaka kumi na tano hadi wakati Mungu alipomwita nabii Hagai. Hagai kwa hakika, alihubiri huko Hekaluni. Yeye aliwaambia watu, *'Je! Huu ndio wakati wa ninyi kukaa katika nyumba zenye mapambo ya mbao, iwapo nyumba hii inakaa hali ya kuharibika?* **(Hagai 1:4).**' Hagai aliwahimiza kuirudia kazi na kujenga upya Hekalu la Mungu.

Nyaraka katika Agano Jipya kutoka kwa mitume zinalingana na mtindo huu. Katika Agano Jipya, kazi ya Mungu ilikuwa kulijenga tena Kanisa la Kristo. Wakati shida zitukiapo ambazo zilikuwa vikwazo kwa kazi ya Mungu, Yeye alimwinua mtume ambaye aliuandika waraka. Waraka wa mtume ulikuwa wa nini? Ni kulilia dhidi ya vikwazo ambavyo vilikuwa vikifungia kazi ya ujenzi wa Kanisa ya Kristo aliyefufuka hadi itakapoondolewa na kazi hiyo kuendelea.

Shida na vizuizi vilivyo zungumziwa na manabii sio zile zile zilizo elezewa katika nyaraka za Agano Jipya. Unapounganisha ujumbe wa manabii na vitabu vya Agano Jipya, yamkini utapata vitabu arobaini vya Biblia ambavyo vina mwongozo wa jinsi ya kuondoa vizuizi na shida ambayo ni pingamizi kwa kazi ya Mungu siku ya leo.

Mungu anataka kutenda kazi yake kupitia watu wake. Na hii ni kweli iliopo siku ya leo kama ilivyokuwa siku za manabii pamoja na mitume. Unapotambua kazi yake Mungu katika sehemu yako ya ulimwengu na pale Mungu amekuweka ili kuitenda, na ikiwa umekumbwa na shida - pingamizi, ikiwa una ushawishi kwamba Mungu hatendi kazi inavyompasa, fanya maombi hadi wakati utailenga pingamizi inayozuia kazi yake Mungu. Utakapofahamu kizuizi chako ni kipi, yaendee Maandiko ya manabii au mitume, kisha mwulize Mungu akupe hekima, neema, na ujasiri wa kutumia ujumbe ule katika mazingira ya shida zile zinazoikumba kazi yake Mungu pale ulipo.

Kupitia manabii na mitume, Mungu atakuonyesha jinsi ya kuondoa vizuizi vinavyo izuia kazi Yake. Ikiwa manabii pamoja na mitume hawakumbani na shida na vizuizi vilivyoizuia kazi ya Mungu katika sehemu uliomo ulimwenguni, inawezekana kuwa katika roho za manabii na mitume, Mungu anataka wewe kuipaza sauti yako kuhusu shida na vizuizi vile hadi zitakapokuwa zimeondolewa na kazi yake kuendelea.

# SURA YA PILI

## 'Kuja Na Kuondoka Kwa Isaya'

Manabii wamegawanywa katika makundi mawili, 'Manabii wakuu' na 'wadogo.' Hii si kusema kwamba 'manabii wakuu' wana nyadhifa kuu kuliko manabii wadogo.' Tofauti yao imo katika kiwango na urefu wa yale waliyoandika. Tunapofikira kuhusu nabii .wakuu' na 'wadogo', nabii 'mkuu' ndiye Isaya kwa kuwa kitabu chake ndicho kilicho kirefu kati ya vitabu vyote vya manabii.

Isaya, alitoka katika nyumba ya Wayahudi ya kifalme. Desturi na historia ya walimu wa Kiyahudi yaani "Manabii" yatueleza sisi kwamba Yeye alikuwa nao uhusiano wa kiukoo naye mfalme Uzia na mfalme Joashi kumpitia baba mzazi. Na kwa kuwa Isaya alihudumu chini yao wafalme kadha, ukoo wake wa kifalme ulikuwa ni tayarisho njema kwa huduma ambayo Mungu alimwitia yeye.

**Baadhi Ya Mtazamo Muhimu Wa Kihistoria**

Ingawa mafunzo haya Biblia ni jinsi ya kuabudu binafsi na uchunguzi wa utendaji wa utendaji wa kutufaa maishani, kuna mtazamo wa kihistoria ambao ni lazima uwe nao ili kuelewa vyema ujumbe wake huyu nabii. Nyakati za kihistoria ambazo hawa manabii waliishi, kuhubiri, kuandika na kuwa na huduma zao, (kuanzia mwaka wa 800 Kabla ya Kuzaliwa kwake Kristo hadi mwaka wa 400 Kabla ya Kuzaliwa kwake Kristo) kulikuwa na falme tatu zenye uwezo mkuu: Falme na miliki kuu ya Ashuru, ambayo iliiteka nyara ufalme wa kaskazini (Israeli); nao milki kuu ya Wababeli ambayo iliwavamia, kuwateka pamoja na kuhamisha wana wa Yuda waliokuwa katika ufalme wa kusini pamoja na Waamedi na Waajemi walioiteka Babeli.

Isaya alipata kuishi nyakati ambapo Ashuri ndio waliokuwa wametawala, kabla yao kuvamia ‘ufalme wa kaskazini na kuteka mji ule mkuu wa Samaria. Makabila kumi ambayo yaliitwa ‘Israeli,’ walichukuliwa mateka na tangu nyakati zile hawajawahi kusikika tena. Mahubiri mengi ya Isaya yalikuwa onyo kwa taifa la kaskazini -Israeli ambalo lilitekwa nyara, kwamba wana wa Ashuru walikuwa wakija kuivamia Israeli kama Hukumu yake Mungu kwa dhambi yao ya kuabudu sanamu.

Baada ya Waashuru kuivamia falme ya kaskazini na kuiteka pamoja na kuhamisha makabila kumi ya kaskazini, waligeukia kusini na kuvaamia ufalme wa Kusini, yaani Yuda. Waliiteka miji arobaini na sita yenye kuta kuu huko Yuda. Majeshi ya Ashuru yalifikia karibu lango kuu la Yerusalemu na kuchukua yamkini watu elfu mbili mateka hadi huko Ashuru. Hata hivyo, wakati walipofikia malango ya mji wa Yerusalemu, Isaya alikuwa kwa wakati huo akiwika kama nabii.

Mfalme Hezekia ndiye aliyekuwa akitawala Yuda wakati huo, na alikuwa mtu wa kiroho mwenye maombezi makuu. Pia yamkini ni mwandishi wa Zaburi kama kumi. Wakati wana wa Ashuru walipofikia malango ya Yerusalemu, mkuu wa jeshi lao aliipaza sauti huku akiwapa changa moto ya vitisho na matusi walinzi waliokuwa juu ya kuta za mji wa Yerusalemu, huku akiwatisha ili Yuda wajisalimishe.

Huku mfalme Hezekia akiendelea na maombi yake kwa Mungu kuokoa maisha ya watu wake, Isaya alipokea ufunuo. Hivyo basi, nabii huyu alikwenda hadi Hekaluni na kumwambia Hezekia kwamba ukombozi utakuja kwa kuwa Mungu alikuwa ameyasikia maombi yake. Isaya alimwambia huyu mfalme, kwamba majeshi ya watu wa Ashuri watapata ujumbe unaosema kwamba wanahitajika kurudi katika nchi yao. Na wakati mkuu wa majeshi angewasili huko Ashuru, angeuawa.

Usiku huo, yamkini askari elfu mia moja na themanini na tano (185,000) walikufa kwa tauni iliyotokea katika kambi yao. Siku iliyofuatia, maiti ziligunduliwa na jeshi lile lililokuwa limehama kambi kurudi kwao nyumbani. Wao walipowasili huko Ashuru, unabii wake Isaya ulitimia wakati wana wake mkuu huyu wa jeshi la Ashuru walimwua. Kulingana na binadamu, unaweza kusema kama haungekuwa ni ushawishi wa huduma ya huyu nabii Isaya, Waashuru wangehamisha watu wote wa ufalme za kaskazini na kusini na kutoweka kabisa.

Isaya anatupa mfano bora katika Biblia kuhusu huduma ya unabii ya kueleza mambo yajayo. Yeye alitabiri kweli kwamba wana wa Uajemi wangevamia milki ya Babeli na kwamba Koreshi Mkuu angetoa amri kwa mateka kurejea katika nchi yao na kujenga Hekalu. Alitaja jina lake Koreshi mara mbili na kutabiri tukio hili kuu katika historia ya Waebrania.

Historia na desturi zinatuambia kuwa wakuu wa Kiyahudi na wale waliokuwepo katika nchi ya uhamisho walimwonyesha mfalme Koreshi Mkuu nakala hii ya Isaya na mwujiza wa unabii uliomshawishi kutoa amri hii ya ajabu. Bali na kuwapa ruhusa ya kurudi makwao, pia alitoa

mali na vyombo vilivyohusika katika ujenzi wa Hekalu. Katika utabiri wake Isaya uliotimika wakati taifa la Uajemi lilipoivamia Babeli, jambo la kwanza ambalo huyu Koreshi alitenda ilikuwa kutoa amri kusema kwamba mateka wote wa Kiyahudi wangeweza kurudi Yerusalemu na kujenga Hekalu lao **(Isaya 44:28 - 45:7; Ezra 1:2-4).**

### Mhubiri Mkuu

Inawezekana kwamba huyu Isaya alikuwa mhubiri mkuu. Kulingana na Yesu, Yohana Mbatizaji ndiye aliyekuwa nabii mkuu kuwahi kuzaliwa na mwanamke **(Luka 7: 28).** Hata hivyo, tunaelezewa kwamba wakati Yohana alipokuwa akihubiri huko nyikani, alihubiri mahubiri ya Isaya **(Luka 3:4).** 'Aliye kuwa nabii mkuu kuzaliwa na mwanamke' alihubiri ujumbe wa Isaya, jambo ambalo linamfanya Isaya kuwa 'Nabii wa manabi.'

Isaya alipata kuhubiri takribani miaka hamsini, au labda sitini. Alipata kuishi nyakati za wafalme watano wa Yuda na sita wa Israeli. Ingawa yeye alikuwa na mengi ya kusema kuhusu yale yangetokea hapo baadaye kwa ufalme wa Kaskazini kutoka Ashuru, huduma yake kuu pamoja na jukumu zake zilikuwa katika ufalme wa kusini wa Yuda.

Ikiwa unataka mtazamo wa ki historia kuhusu Isaya, kwa uangalifu hebu tazama mistari ya kufungua kuhusu unabii wake. Vitabu hivi vya unabii wakati mwingi huweka kumbukumbu ya nyakati na huduma za nabii kulingana sawa na wafalme waliokuwepo wakati huo. Baadhi ya wafalme fulani ambao walikuwa wakitawala wakati wa uhai wake nabii Isaya, walikuwa wema ilhali wengine walikuwa waovu. Mmoja wa wale waliokuwa waovu ni mfalme Manase, ambaye historia inatuambia kwamba alimfanya Isaya kuuawa kwa kukatwa kuwili kwa msumeno. Wasomi huamini kifo chake nabii Isaya ndicho kinachozungumziwa katika sura ya imani kwenye nakala iliopo katika Biblia inapotaja kweli kuhusu baadhi ya mashujaa wa Agano la Kale wa Imani 'waliokatwa kuwili kwa msumeno **(Waebrania 11:37).'**

### Kugawa Kitabu

Kuna njia nzuri ya kugawa kitabu hiki cha Isaya.Sura za kwanza thelathini na tisa ni ujumbe wake Isaya akiwaonya watu wa Mungu kuhusu uvamizi na kutekwa nyara na wana wa Ashuru. Sura za mwisho ishirini na saba ni ujumbe kuhusu uponyanji na faraja. Ni kana kwamba sura thelathini na tisa za kwanza za Isaya ni 'upasuaji wa kiroho,' ilhali zile ishirini na saba ni uponyaji ufuatao 'upasuaji.'

Jinsi sura hizi sitini na sita za kitabu cha Isaya zilivyogawany'wa, zimewashawishi wengine kulinganisha kitabu hiki na Biblia yenyewe. Hebu linganisha matukio haya yanayo fanana: kuna sura sitini na sita katika kitabu cha Isaya; ilhali kuna vitabu sitini na sita katika Biblia. Isaya kimegawanyíwa katika sehemu mbili, zikiwemo sura thelathini na tisa na ishirini na saba. Biblia imegawanywa katika sehemu mbili, sehemu mmoja ikiwa ni Agano la Kale yenye vitabu thelathini na tisa huku Agano Jipya likiwa na vitabu ishirini na saba. Sehemu ya kwanza ya Isaya inasomeka kama Agano la Kale, ikiwa maonyo mengi na ujumbe wa kuwarudi na

inadhihirisha hali ya kweli ya mwanadamu pamoja na suluhisho ambalo anaweza kupata kutoka kwa Mungu.

Sehemu ya pili ya Isaya ni kama 'Agano Jipya' ambayo hutoa faraja na tumaini kwa watu ambao wana ufahamu haja zao za mwokozi kwa kuwa wamesoma 'Agano la Kale' sehemu ya Isaya ambayo ilionyesha njia yake Mwokozi. Agano la Kale linaanza kwa swali hili, 'Uko wapi? **(Mwanzo 3:9).'** Nalo Agano Jipya linaanza kwa swali 'Uko wapi? **(Mathayo 2:2)**. Sehemu hizi mbili za Isaya hutufanya kutambua haja ya mwokozi na kutujulisha kwa mtumishi aliyeteseka katika sura ya hamsini na tatu.

**Mwito Wa Isaya**

Vifungu viwili katika kitabu cha Isaya hutusaidia kumfahamu vyema, pamoja na huduma na ujumbe wake. Mojawapo ya kifungu hicho ni sura ya sita, ambayo ni maelezo ya mwito, na kuagizwa kwake Isaya. Inawezekana pia kuwa ni maelezo ya kubadilishwa kwake Isaya. Katika Maandiko, watu wote wake Mungu huwa na jinsi ya kumjia Mungu ambako kuna maana, hivi kwamba waweze kuwa na kumwendea kwenye maana. Sura ya sita ya Isaya ina maelezo kuhusu ushuhuda wake pamoja na kuagizwa kwake na Mungu ili apate kwenda.

Huku Isaya akipata ushuhuda wa kumwendea Mungu, yeye anamsikia akisema, *'Ni nani nitakayemtuma? Na ni nani atayekwenda kwa ajili yetu? (8).'* Kwa kujibu, Isaya anaeleza kujitolea kwake kwa maneno haya: *'Mimi hapa, nitume mimi!'* Mtindo huu umefafanuliwa sana katika Maandiko. Watu wote wa Mungu ambao humjia husikia agizo na kwenda kwa niaba ya Mungu.

Mungu alimweleza kuwa, *'Isaya, watu hawatakusikiza wewe. Sababu yako kutenda sio kwamba watu wakapate kuongoka. Wao tayari wamechagua kuniasi mimi. Lakini hata hivyo, Mimi nakutaka wewe kuwaendea, kwa kuwa Mimi nataka wao wausikie ujumbe wangu.'* Ni jambo lililo gumu sana kuwa mhubiri. Hebu fikiria kuwa mhubiri kwa miaka hamsini na sita pasi wepo na mtu ye yote kuhusika na mahubiri yako!

Kujitolea kwake Isaya kwa mwito huo ni kwa kushangaza mno. Yeye aliuliza kwa urahisi, 'Ee Bwana hata lini?' Naye Mungu alimjibu, *'Hata miji itakapokuwa ukiwa, haina wenyeji, na nyumvba zitakapokuwa hazina watu, na nchi hii itakapokuwa ganjo kabisa; hata Bwana atakapowahamisha watu waende mbali sana, na mahame yatakapokuwa mengi ndani ya nchi* **(6:11,12).'** Kujitolea kwa Isaya ni mfano bora kwetu sote. Kwa hakika kujitolea kwa manabii kulikuwa ujumbe mkuu waliouhubiri. Wao walikuwa wameingia katika maagano na Mungu. Mungu aliwaambia kwenda, nao wakatenda hivyo. Na walipokuwa katika kwenda, jambo la muhimu lilikuwa kwamba ni waaminifu kwa Mungu na walitenda yale ambayo Mungu aliwaagiza kutenda.

Wajibu wetu ni kutenda yaleo Mungu ametuitia na kutuagizia. Matokeo ya utiifu ni kazi ya Mungu. Ni Mungu peke yake, Roho Mtakatifu, ambaye anaweza kuleta matokeo. Wajibu wetu ni

kuwa watiifu tu. Kuzalisha kwa matunda ni wajibu wake Mungu. Wajibu wetu ni kutenda yale Mungu ametuitia.

## SURA YA TATU

## ‘ Mahubiri Ya Kimasihi’

Kuna jumbe za kimasihi katika unabii wa Isaya zaidi kuliko kitabu kingine cha unabii. Isaya amenakiliwa mara nyingi katika Agano Jipya kuliko nabii ye yote katika Agano la Kale. Unaposoma kitabu cha Isaya, tazama jumbe za kimasihi katika unabii wake. Katika Isaya, utaupata unabii huu kuhusu majina ambayo Masihi atajulikana punde atakapo kuja: *‘Jina lake ataitwa Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa Milele, Mfalme wa amani* **(Isaya 9:6)**.’ Isaya alidhihirisha wazi kabisa kwamba Masihi angekuwa Mungu katika mwili wa mwanadamu, au ‘Imanueli, maanake, ‘Mungu pamoja nasi **(Mathayo 1:23).’**

Isaya anatueleza hali kamili ya Roho ambaye atadhihirishwa kupitia Masihi wakati atakapokuja: *‘Basi litatoka chipukizi katika shina la Yese, na tawi lita-kalo-toka katika mizizi yake litazaa matunda. - Na roho ya Bwana atakaa juu yake, roho ya hekima na ufahamu, roho ya shauri na uweza, roho ya maarifa na ya kumcha Bwana* **(Isaya 11:1-3)**.’ Haya yana nakiliwa katika kitabu cha Ufunuo, ‘Roho saba wa Mungu **(Ufunuo 3:1; 4:5; 5:6).’**

Kwa kuwa nambari saba inawakilisha ukamilifu katika Biblia, na jinsi ambavyo Isaya anatueleza kuhusu kuja kwa Masihi, yale ambayo anasema ni, *‘Masihi atakuwa dhihirisho timilifu la Roho wake Mungu. Masihi atakuwa dhihirisho la hali ya kiroho ya Mungu kwa njia saba. Katika maisha yake atatokea Roho wa maarifa, Roho wa ufahamu, Roho wa Hekima, Roho wa Ushauri, Roho wa Uweza, Roho wa Ibada, na Roho wake Bwana.’*

Unaposoma Injili zile nne, je! Ni picha gani iliyo katika mawazo yako? Kulingana na Isaya, hivi ndivyo Masihi atakavyokuwa (alivyokuwa): Maisha yake yatadhihirisha Roho wa maarifa na Roho wa ufahamu. Yeye atajua na kufahamu Neno la Mungu kikamilifu. Roho wa hekima inamaanisha kutekeleza maarifa yake, hivyo basi, Yesu pia atadhihirisha Roho wa hekima atakapokuwa akitekeleza Neno la Mungu katika maisha yake mwenyewe na ya watu wengine. Hii inamaanisha kwamba atamdhihirisha Roho wa Ushauri. Na atakapotenda hivyo, kutakuwepo na uwezo wa kubadilisha maisha na huduma Yake. Hii ikidhihirisha Roho wa nguvu na uwezo.

Mwishowe, Isaya anatabiri Masihi atadhihirisha na kuonyesha Roho ya Ibada, au kumcha Bwana. Yeye anaongeza maelezo zaidi atafurahia dhihirisho hili la mwisho la Roho ya kuabudu. Unaposoma Injili, utagundua kwamba, wakati Yesu hakuwa akiwahudumia watu, Alikuwa katika maombi na kuabudu. Hebu soma vitabu vya Injili kisha utazame fungu hili la Roho saba wake Mungu, ambao ni utimilifu wa dhihirisho la Roho aliyetimilika katika maisha ya Yesu.

Katika mwisho wa karne ya ishirini, kumekuwa na ufufuo na wa Roho Mtakatifu. Tunapotafsiri ushuhuda wa Roho Mtakatifu, huwa tunafanya migawanyiko na vurugu nyingi kwa kuwa tunafanya makosa katika njia ile ambayo tutataja ushuhuda wetu na Roho Mtakatifu. Kwa mfano, je! Umewahi kusikia watu ambao huwataja wengine kama waaminifu, wachungaji au Makanisa yaliojazwa na Roho Mtakatifu? Hii ni kusema kwamba kuna aina mbili ya watu waaminifu, wachungaji na Makanisa. Kuna waaminifu, wachungaji, na Makanisa yaliojawa na Roho Mtakatifu na pia kuna waaminifu, wachungaji na Makanisa ambayo hayajajazwa na Roho Mtakatifu.

Je! Haya ndiyo yale Biblia inayomaanisha wakati inapoeleza kuhusu mwaminifu aliyejazwa na Roho? Waaminifu wote wameagizwa: ‘kujazwa na Roho **(Waefeso 5:8).’** Maanake katika lugha asili ni kujazwa na Roho.’ Agizo hili katika lugha ya Kiyunani, mtindo wake dhahiri ni Agizo wala sio jambo lenye uchaguzi kwa mfuasi wa kweli wake Yesu Kristo.

Je! Maana ya kujazwa na Roho Mtakatifu ni nini? Sisi tumeelezwa katika Kitabu cha Matendo kwamba Petro, *‘akiwa amejazwa na Roho,’* alihubiri ujumbe mkuu siku ile ya Pentekoste. Baadaye tunasoma *‘Petro, akiwa amejazwa na Roho,’* alihubiri mara nyingine na maelfu ya watu wakaokolewa. Na kwa mara nyingine, hapo baadaye tunasoma *‘Petro, akiwa amejawa na Roho,’* alitenda hiki na kile. Yamkini, Maandiko haya yanatueleza Petro alikuwa amejawa na Roho.Je! Hakika alijazwa na Roho?

Roho Mtakatifu sio kitu kama maji. Roho Mtakatifu ni mtu, na yamkini tunaye utu wa Roho Mtakatifu katika maisha yetu au sivyo. Swali kuu sio, ‘Ni kiasi kipi cha Roho Mtakatifu tulicho nacho?’ ila ni ‘Roho Mtakatifu ana kiasi kipi kutoka kwetu?’ Wakati ambapo tumejitolea kikamilifu kwake, ndipo huwa tumejawa na Roho Mtakatifu.

Mwamini aliyejawa na Roho Mtakatifu ni yule ambaye anaongozwa na Roho Mtakatifu. Kabla ya Paulo kutushauri kuwa hivyo, kujawa naye Roho Mtakatifu, yeye aliandika haya: *‘Msilewe kwa mvinyo, ambamo ndani mwake mna ufisadi, bali mkajazwe naye Roho Mtakatifu* **(Waefeso 5:18).’** Kama jinsi alivyo mlevi, sisi pia tunahitajika kuwa chini ya ushawishi wake Roho Mtakatifu, au chini ya uongozi wake Roho Mtakatifu.

Unabii huu wenye kuvutia wake nabii Isaya unahitaji kutufunza kwamba hatupaswi kuogopa kujawa na Roho Mtakatifu. Kwa sababu, ikiwa tumejawa na Roho Mtakatifu, na ikiwa tunatawaliwa kikamilifu na Roho Mtakatifu, na ikiwa tunadhihirisha utu wa kweli wake Mungu na jinsi alivyo katika Roho Mtakatifu, basi tutakuwa kama Yesu Kristo wakati alipodhihirisha na kuonyesha maeneo haya saba ya Roho wa Mungu.

Isaya anatuambia kwamba Yesu Kristo alikuwa dhihirisho kamili ya Roho wake Mungu. Yesu Kristo alitawaliwa asilimia mia mmoja na Roho wakati wote, au kwamba alikuwa amejawa na Roho kila mara. Roho wa Mungu kwa ukamilifu wote alidhihirika katika maisha ya Yesu Kristo. Na Je! Yeye alifanana vipi? Soma vitabu vinne vya Injili upate kijionea mwenyewe. Je! Mtu ye yote anaweza kusoma injili bila kutaka kuwa kama Yesu? Kwa hakika, maisha yake ndiyo kielelezo ambacho sote tunahitajika kuiga na kuishi tunapo udhihirisha utu wa kweli wa Mungu wetu - Ambaye ni Roho.

**Njia Kuu Ya Mungu**

Katika Isaya sura ya 40 tunapata unabii mwingine wa Kimasihi wenye kuvutia: *'Sikiliza, ni sauti ya mtu aliaye, Itengenezeni nyikani njia ya Bwana; Nyosheni jangwani njia kuu kwa Mungu wetu. Kila bonde litainuliwa, Na kila mlima na kilima kitashushwa; Palipopotoka patakuwa pamenyoka, Na palipoparuza pata-sawa-zishwa; Na utukufu wa Bwana utafunuliwa, Na wote wenye mwili watauona pamoja; kwa kuwa kinywa cha Bwana kimenena haya* **(3-5).'**

Wakati Yohana Mbatizaji alipokuja akihubiri ujumbe wake Isaya, alihubiri **(Luka 3:4-6).** Huu ni mojawapo wa jumbe kuu za nabii Isaya. Yeye anahubiri kwamba Mungu atakuja humu duniani katika utu wa mwanawe, Masihi. Isaya analinganisha tukio hili na mfalme aliyefunga safari. Ikiwa mfalme alikuwa amifunga safari kukitembelea kijiji fulani cha mbali, raia wake wangelihitajika kuijenga njia ambayo angesafiria. Nayo njia ile ingeitwa, 'Njia kuu ya mfalme.' Unapojenga njia kuu, kuna mambo manne ambayo unahitajika kutenda: Milima na vilima kushushwa, bonde kuinuliwa, palipo-potoka kunyoshwa na palipo-paruza kusawazishwa.

Isaya anatumia mfano huu wa kila siku na kusema, *'Mungu anataka kusafiri humu ulimwenguni, lakini anahitaji njia kuu atakayosafiria. Njia kuu ambayo Mungu atatumia kuja ulimwengu itakuwa maisha ya Mwanawe. Maisha ya Mwanawe Mungu yataweza kutajawa kama milima ya kiburi imeshushwa, na mabonde au sehemu zilizo na ukiwa zimejawa, sehemu za dhambi zilizo potoka zimenyoshwa, naye Mwana wa Mungu atakumbana na sehemu zilizoparuza na kuzisawazisha. Hapo ndipo kutakapokuwepo na njia kuu ambayo Mungu atasafiria huku ulimwenguni na wote wenye mwili watauona wokovu na utukufu wake kupitia njia hiyo kuu.'*

Kwa sababu Yesu alikuwa akituonyesha jinsi ya kuishi, hii inamaanisha kwamba maisha yetu yanahitajika kuwa njia kuu yake Mungu. Hebu nikupe changa moto hii upate kufanya maombi haya, 'Mungu, fanya maisha yangu kuwa njia kuu ambayo Wewe unaweza kutembelea ulimwengu huu.' Punde tu, utakapofanya maombi hayo, usishangae wakati Mungu atakapotuma, 'tinga tinga kubwa' kuanza kazi ya kuishusha milima na vilima vya kiburi chako, na kujaza mabonde ya utupu wako, kuzinyosha njia zilizopotoka kwa dhambi na kusawazisha palipoparuza. Wakati tufanyapo maombi haya, Mungu ataning'iniza onyo juu yetu lenye kusema, ëIlani: Mungu Atenda Kazi!'

**Sera Au Maongozi Ya Nazareti**

Ujumbe mwingine wa ajabu wake Isaya unapatikana katika sura ya sitini na moja. Huu ni unabii wa Kimasihi kuhusu huduma ya Yesu kwa jamii. Wakati Yesu alipoanza huduma yake ya miaka mitatu kwa jamii, alifanya hivyo kwa maongozi au sera ambalo wasomi wengi wanalitaja kama 'Sera ya Nazareti.' Yesu alikwenda katika Sinagogi kijijini mwao na kuitisha chuo cha nabii Isaya. Akakifungua chuo kile na kupatafuta pale palipoandikwa maneno haya: *'Roho ya Bwana Mungu I juu yangu; kwa sababu Bwana amenitia mafuta niwahubiri wanyenyekevu habari njema; alinituma ili kuwaganga waliovunjika moyo, kuwatangazia mateka uhuru wao, na hao waliofungwa habari za kufunguliwa kwao. Kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa.' Akakifunga kile chuo na baada ya kuketi chini akasema, 'Leo Maandiko haya yametimia masikioni mwenu* **(Isaya 61:1,2; Luka 4:18)**.'

Ukilinganisha unabii katika kitabu cha Isaya sura ya sitini na moja na yale yalionakiliwa na Bwana katika kitabu cha Luka, sura ya nne, utatambua kwamba aliachia nakala yake Isaya katikati mwa sentensi. Isaya anaendelea kusema, 'na siku ya kisasi cha Mungu wetu.' Yesu hakusoma sehemu hiyo ya msitari kwa kuwa iligusia mjio wake wa pili. Masihi atarudi kwa mara nyingine na kulipiza kisasi kwa maadui zake Mungu. Yesu aliachia katikati mwa sentensi ile na kukirudisha chuo kwa mtumishi kwa kuwa alikuwa akitanza sera yake kwa miaka mitatu ijayo katika huduma iliyofuatia siku ile. Baadaye akasema, *'Leo Maandiko haya yametimia masikioni mwenu* **(Isaya 61:1,2; Luka 4:18-21).'**

Yesu alikuwa akisema, *'Roho wake Mungu yu juu yangu Mimi. Yeye amenipaka mafuta ili kuwahubiria walio maskini.'* Hawa maskini walikuwa katika hali ya upofu. Upofu ulimaanisha kwamba wao hawakuwa na mbele wala nyuma. Pia walikuwa maskini kwa kuwa walikuwa ni wafungwa, kumaanisha kwamba hawakuwa huru. Pia walikuwa maskini kwa kuwa walikuwa wamavunjika mioyo yao.

Siku ile katika Sinagogi kuu kijijini mwake, Yesu alitangaza kwa ufasaha mwingi: *'Huduma yangu inaelekezwa kwa vipofu, waliofungwa, waliovunjika na watu waliojehuriwa mioyo yao. Ninapotangaza Injili yangu kwa watu hawa, vipofu watapata kuona, waliofungwa watakuwa huru na wenye kuvunjika na kuumia watapata uponyaji.'* Baada ya kufanya tangazo hilo kuu, Yesu alianza huduma yake ya miaka mitatu kwa jamii.

Manifesto ya Nazareti ni njia ya kuvutia ambayo kupitia kwake unaweza kutazamia vema huduma ya Yesu Kristo katika kila kitabu kati ya vitabu vinne vya Injili, hasa katika Injli ya Luka. Wakati Yesu, ambaye alikuwa Mungu pamoja nasi, alipotaka kufanya tangazo la sera yake, na kile alichokuwa akitenda, sawa na Yohana Mbatizaji, pia aliuhubiri ujumbe wa Isaya.

Unaposoma Injili zote nne, hebu tazama kwa makini yale Yesu aliyotenda kwa miaka mitatu baada ya kutangaza sera ya mwongozo wake huko Nazareti. Aliwapa vipofu uwezo wa kuona tena. Ingawa aliwafanya vipofu halisi kuona tena, pia kupitia huduma yake ya mafundisho, aliwafungua vipofu wa kiroho wapate kuona tena. Alikuwa na huruma nyingi kwa makutano kwa kuwa wao walikuwa kama kondoo ambao hawafna mbele wala nyuma. Kuwapa vipofu wa kiroho kuona tena, hakika kulikuwa mfano mkuu ulioambatana na huduma ya mafundisho.

Katika huduma ya ushauri, aliwafanya wafungwa huru. Yeye aliwaahidi wale waliokuwa wamefungwa kwamba atawaongoza kwa kweli ambayo itawaweka huru ikiwa watamfuata (**Yohana 8:30-35).**

Ikiwa wewe ni kipofu kiroho, na ikiwa umevurugika na haufahamu mbele wala nyuma, huduma yake Masihi inaelekezwa kwako. Lengo lake kuu ni kukutana na mahitaji yako, na kuona kwamba umepokea tena kuona. Ikiwa wewe hauko huru, ikiwa wewe ni mfungwa wa tabia ye yote na ikiwa wewe unatawaliwa na tabia, tamaa na uchu mbovu, basi huduma ya Masihi inaelekezwa kwako. Yeye alikuja kwa watu kama wewe. Yeye anataka kukufanya huru. Ikiwa umechubuka na kuvunjika moyo kwa kuwa maisha ni magumu kwako, basi kumbuka kwamba Yesu alikuja kwa ajili ya watu kama wewe. Yeye anapenda wewe uponywe. Yeye anataka kukufanya huru.

Na ikiwa tayari una ushuhuda wa muujiza wa wokovu ambao Yesu na Isaya wanataja katika sera ya mwongozo wa huduma yake Masihi, basi unapoenenda ulimwenguni na kushirikiana na watu, kumbuka kwamba huduma yake Yesu pia inaelekezwa kwa watu wale. Jiulize mwenyewe, 'mimi ni kipofu? Mimi nimevunjika?' Kristo ambaye yupo ndani yako anataka kuwa na huduma katika maisha yao kama vile alivyo katika maisha yako. Yeye anataka sasa kuwa na huduma kupitia kwako.

Alipokuwa na wanafunzi wake nyakati za mwisho kabla ya kufa msalabani, Yesu aliwaambia kwamba Atamtuma Mfariji, Roho Mtakatifu, ambaye atakaa ndani mwao. Hii ndio maana iliyopo katika Agano Jipya wakati inapotuambia sisi, wafuasi wake Yesu Kristo, Kanisa Lake kuwa, 'tu mwili wake Kristo.' Yeye anaishi ndani yetu. Sisi tu mikono yake, miguu yake, utu wa mwili ambao Yeye anajidhihirisha mwenyewe siku ya leo, akiwapa kuona walio vipofu, uhuru waliofungwa, uponyaji waliovunjika na kuchubuliwa katika ulimwengu huu.

**Mwokozi Anayeteseka**

Eneo lingine la mahubiri ya Kimasihi kutoka kwake Isaya linatilia mkazo juu ya kifo chake Yesu Kristo. Sura ya hamsini na tatu ya Isaya ni mmojawapo ya sura zilizo kuu katika Biblia kuhusu maana ya kifo chake Yesu Kristo. Katika sura hii yenye kuvutia, Isaya anafungua na swali hili, *'Ni nani aliyesadiki habari tuliyoileta? Na mkono wa Bwana amefunuliwa nani?'* Kumbuka kwamba, Isaya alikuwa ameagizwa kuhubiri kwa watu ambao hawangemwamini. Yeye alifahamu kwa wazi kabisa kwamba wakati Neno la Mungu likihubiriwa, na kama Roho Mtakatifu hataliangazia na kufunua maana yake kwa watu, wao hawangelielewa au kuliamini.

Kile ambacho Isaya alikuwa akiuliza ni, *'Ni nani ambaye kwa hakika anaelewa maana ya kifo cha Yesu?' Kina kikuu cha mafunzo yake Isaya katika sura hii kinapatikana katika msitari wa sita: 'Sisi sote kama kondoo tumepotea; Kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe; Na Bwana ameweka juu yake Maovu yetu sisi sote.' Ni katika njia gani ambayo Mungu aliweka uovu wetu juu yake Masihi? 'Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona (5).'*

Msitari wa sita unafungua na kufunga kwa maneno haya 'sisi sote.' Mara ya kwanza Isaya anatumia maneno 'sisi sote' kusema kuwa tu kama kondoo. Je! Maneno haya yanajumuisha wewe? Yamkini kwamba unaweza kukumbuka kwamba katika **Zaburi 23** imeandikwa, *'Bwana ndiye Mchungaji wangu. Hunilaza katika majani mabichi* **(1-2).**' Wakati tunapokiri kwamba Bwana ndiye Mchungaji wetu, pia tunakiri kwamba tu kondoo wa malisho yake. Basi hapa katika msitari huu tunapata mahali pengine Maandiko yanatuhimiza kukiri kwamba tu kondoo. Sisi sote tu kondoo waliokwenda kila mmoja kwa njia yake. Maelezo mengine ni kwamba sisi sote, tu wenye dhambi; tumezigeukia njia zetu wenyewe.

Mara nyingine Isaya anatumia maneno 'Sisi sote' anatupatia Habari Njema. *'Bwana amemtweka yeye maovu yetu sote.'* Je! Wewe unaamini kwamba umejumuishwa katika 'sisi sote' ya mwisho ya Isaya? Ikiwa unakiri kwamba upo katika kundi kile cha kwanza cha ësisi soteí na pia unakiri kwamba upo katika kundi la mwisho la ësisi soteí, ni wazi kwamba unakiri na kuikumbatia maana ya kifo chake Yesu msalabani kwa ajili ya maisha yako. Na hivyo, unaweza kuwa na ushuhuda wa wokovu ambao ulidhihirishwa wakati Mungu alipotumia maisha yake Mwanawe kama Njia Kuu ya kututembelea duniani.

# SURA YA NNE

# Unabii Wa Yeremia

**'Mfululizo Wa Kilio'**

Nabii mkuu anayefuatia katika Agano la Kale ni Yeremia. Yeye anatajwa kama 'nabii mwenye kulia' kwa kuwa alikuwa ni mwenye kulio wakati mwingi. Hakika, unabii wake Yeremia ni 'mfululizo wa kilio.' Kwa hakika ni vigumu sana kuwa na utaratibu mwema wa kitabu cha Yeremia kwa kuwa kilio au maombolezi hayana utaratibu wo wote. Baada yake kulia katika sura hamsini na mbili, Yeremia aliandika shairi au tenzi la kushangaza ambalo linafuatia unabii wake

linalojulikana kama ‘Maombolezo’, maanake ‘vilio.’ Katika tenzi hii ya mombolezo ambalo ni mojawapo ya Maandiko yenye kuvutia, Yeremia azidi kulia.

**Baadhi Ya Mitazamo Ya Kihistoria**

Yeremia alikuwa akilia kwa sababu gani? Sababu gani iliyomfanya kufedheheshwa hivyo? Uchungu wa moyo wake ulikuwa upi? Ili kujibu maswali haya, ni lazima ufahamu historia na mazingira ya nyakati ambazo huyu nabii alipata kuishi, ambazo kwa hakika zilikuwa za kusisimua sana pamoja na kuhubiri na kuandika unabii huu ambao tunataja kama ‘Kitabu cha Yeremia.’

Katika mistari ya kufungua, tunasoma nabii huyu alianza huduma yake mwaka wa thelathini wa utawala wa Mfalme Yosia na kuhudumu chini ya enzi ya Zedekia, miaka arobaini na moja. Yeye alianza huduma yake wakati utawala wake mfalme mwema Yosia, mfalme wa Yuda. Katika utawala wa enzi yake Yosia, baadhi ya wajenzi waliokuwa wakifanya ujenzi katika Hekalu waligundua baadhi ya vyuo vya Neno la Mungu. Watu wa Mungu walikuwa mbali naye kwa hali ya kiroho hivi kwamba walikuwa wamesahau Maandiko, au sheria yake Mungu, hata hawakufahamu kama ilikuwepo. Wafalme wengine wanaotajwa katika mistari ya kwanza ya Yeremia ni wale waliofuatia uongozi wake Yosia ambao wahuzishwa na kuanguka kwa Yerusalemu kwa mikono ya utumwa wa Babeli.

Kuanguka kwa Yerusalemu kulikuwa janga lililodumu kwa muda wa miaka ishirini. Wakati wa kwanza Yerusalemu ilipoanguka dhidi ya uvamizi, Yehoiakimu ndiye alikuwa mfalme. Yeye alisalimu amri kwa majeshi yake Nebukadreza, na akapata kumtumikia Nebukadreza akiwa huko Yerusalemu kwa muda wa miaka mitatu. Nebukadreza alipouteka mji wa Yerusalemu, majeshi ya Babeli yaliingia ndani mwake. Nao Wayahudi walilazimishwa kuwatumikia Wababeli pamoja na kuwalipa kodi. Hata hivyo, baada ya miaka mitatu, Yehoikimu aliasi, na hivyo majeshi ya Babeli yakauteka mji wa Yerusalemu kwa mara ya pili. Baada ya Yerusalemu kutekwa kwa mara nyingine, Yekonia mwanawe Yehoyakimu alikuwa angali mtoto mdogo, hivyo alijisamu amri kwa mara nyingine. Wakati huu Wababeli waliwachukua watu wengi wa Yuda hadi Babeli kama mateka.

Yekonia alipousalimisha mji kwa mara ya pili, ndugu yake Zedekia alikuwa tayari amefanywa ‘mfalme kibaraka’ au kaimu mfalme maanake alitawala kwa jina tu kote Yerusalemu. Yeye alitawala hivyo miaka kumi na moja, kisha naye akaasi dhidi ya Babeli. Kwa wakati huu, Wababeli waliharibu kabisa mji wa Yerusalemu. Hapakuwepo nalo jiwe lililoachwa juu ya lingine. Mara hii ya tatu ya uvamizi dhidi ya mji wa Yerusalemu, Wababeli walichukua watu wote mateka hadi Babeli isipokuwa wale waliokuwa wakongwe, wagonjwa, wanyonge, pamoja na yule nabii mwenye kulia au kuomboleza, yaani Yeremia.

Katika utawala wake Yosia, Mungu alimpa Yeremia ufunuo wa unabiii kuhusu janga litakalotokea. Alianza kuhubiri uvamizi kutoka Babeli ungelitokea, na utumwa chini ya kongwa la Babeli ulitokea kwa sababu ya dhambi za watu. Hii ilikuwa hasa kwa sababu ya ibada zao za sanamu, na pia dhambi zao zote zilizotokana na kuasi pamoja na kutolitilia maanani Neno la Mungu.

Hapo mwanzoni, ujumbe wake Yeremia na manabii wengine ulikuwa: *‘Ikiwa watu wangu, walioitwa kwa jina langu, wataji-nyenye-kesha, na kuomba, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao mbaya; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao, na kuiponya nchi yao* **(2 Mambo ya Nyakati 7:14)**.’ Lakini wakati watu hawakutilia maanani mahubiri haya, ujumbe wao manabii uligeuka. Kisha manabii kama Yeremia wakahubiri, *‘Hukumu ya Mungu yaja. Na hakuna njia ya kuiepuka!’*

**Mtu Aliyechukiwa**

Wakati utekaji nyara wa Yerusalemu ulipoanza, Yeremia aliuhubiri ujumbe ambao haukuwafurahisha wengi. Alifanyika mtu aliyechukiwa miongoni mwa manabii. Yeye alikuwa na ujumbe wenye kuwili. Sehemu ya kwanza ya ujumbe huu ilikuwa kuhusu uvamizi na utekaji nyara ambao haungebadilishwa. Nayo sehemu ya pili ilikuwa ya tumaini. Tofauti na utekaji na uvamizi

wa ufalme wa kaskazini (Israeli), manabii wale waliotabiri kuhusu uvamizi kutoka kwa Babeli dhidi ya ufalme wa kusini (Yuda) walikuwa na ujumbe wa tumaini ambao ni: *'Miaka sabini baada ya kuchukuliwa mateka huko Babeli, nyinyi mtarudi.'*

Yeremia aliamini na kuhubiri ujumbe wa tumaini kwa nguvu nyingi, wakati majeshi ya Babeli yalipoanza kuzingira mji wa Yerusalemu, alihubiri kuwa, *'Huu ndio mpango wake Mungu na hutabadilishwa. Na itakuwa vema kama mkijitolea na kujisalimisha wenyewe kwa Nebukadneza. Nendeni huko Babeli, kwa kuwa mapema mwendopo kule, ndipo mtarejapo mapema.'*

Kwa kuwa Yeremia alihubiri kwamba watu wa Yuda wanahitajika kujisalimisha, wao walimchukia. Wao waliutaja ujumbe wake kama uasi na usaliti, na kwa njia nyingine ilikuwa ni ukweli. Wao walimtupa ndani ya kisima kilichojaa matope. Walimwacha mle ndani kwa uchafu na panya bila chakula.

**Mfinyanzi Na Udongo**

Yeremia pamoja na wenziwe wangetenda jambo lo lote kuhakikisha ujumbe wao umewafikia watu. Wao walieleza wazi yale waliokuwa wakitaka kuwasilisha, wakati mwingine kupitia kile kinachotajwa kama 'mahubiri ya mifano au ishara.' Kwa mfano, Yeremia alikuwa na ujumbe mkuu wa mifano na ishara katika sura ya kumi na nane ulioitwa 'chombo kilichofanywa upya.' Yeremia alitabiri kwamba Mungu alikuwa amemwambia kwenda katika nyumba ya mfinyanzi. Wakati alipokuwa mahali pale, alimtazama yule mfinyanzi akitengeneza chombo. Mfinyazi yule alikuwa akijaribu kutengeza chombo chenye kuvutia, lakini chombo hakikutokea jinsi alivyotaka. Kwa hasira dhidi ya chombo kile, huyu mfinyanzi alikitupa chini na kukivunja-vunja. Alichukua tena ule udongo na kufinyanga kisha kutengeneza chombo kingine tofauti.

Wakati Yeremia alipokuwa akiuhubiri ujumbe huu, alikuwa akisema kuwa, *'Ninyi ni kama chombo cha mfinyanzi ambacho Mungu ambaye ndiye Mfinyanzi anatengeneza. Nanyi hamfanyiki jinsi anavyotaka, hivyo basi, Yeye anawaadhibu. Mungu atawachukua ninyi hadi Babeli, na kuwafanya upya, na hapo baadaye awarudishe kutoka huko kama vyombo vipya na tofauti kabisa.'*

Matumizi ya kibinafsi kwa hakika ni dhahiri. Wakati mwingi maisha yetu hayaambatani na jinsi Mungu anavyokusudia. Hivyo basi, inambidi Mungu kutufanya upya tena. Je! Wewe unajihisi hivi? Mara moja maisha yako husambaratika. Nawe unajihisi kana kwamba umetupwa kwenye tope la udongo nakutengenezwa upya. Yale mabadiliko kutoka chombo cha kwanza hadi kipya yanaweza kuwa ya kuumiza, lakini baada ya chombo kutengenezwa, huwa chenye utukufu! Jinsi mtume Paulo alivyoandika, 'Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita; tazama! Yamekuwa mapya **(2 Wakorintho 5:17).**'

Katika kitabu cha Yeremia tunahitaji kutafuta matumizi ya mahubiri ya nabii mkuu. Kuna wakati ambapo Mungu anahitaji kutuadhibu na kutufanya kuwa vyombo vipya. Wakati matokeo ya dhambi zetu hayawezi kuzuiliwa na makofu hayawezi kuondolewa, sisi tunahitaji kufanywa vyombo vipya kabisa kama ilivyo katika ujumbe wake Yeremia juu ya mfinyanzi wa vyombo. Sikitiko ni kwamba wengi wetu hatutafuti wala kumwuliza Mungu kubadilisha maisha yetu, kama watu wale waliokataa kutilia maanani mahubiri yake Yeremia.

**Chombo Kilichoharibiwa**

Siku moja Mungu alimwambia Yeremia kununua chombo kikubwa, chenye thamani kuu, na kuchukuwa baadhi ya wakuu pamoja na makuhani, na kwenda nao hadi kwenye lango la vyombo vilivyovunjika. Watu hao walikuwa makini huku akichukua kile chombo na kukivunja-vunja! Baadaye Yeremia aliuhubiri: *'Ndipo hapo utalivunja gudulia lile, mbele ya macho ya watu wale waendao pamoja nawe, na kuwaambia, Bwana wa majeshi asema hivi, Hivyo ndivyo nitakavyowavunja watu hawa na mji huu, kama mtu avunjavyo chombo cha mfinyanzi, kisichoweza kutengenezwa tena na kuwa kizima; nao watazika watu katika Tofethi hata hapatabaki mahali pa kuzika* **(Yeremia 19:10-11).'**

**Unabii Wa Kimasihi**

Yeremia anapotangaza ujumbe wake wa kutekwa na baadaye wa tumaini, kama Isaya, anachanganya unabii wake kuhusu kurudi kwa mateka na unabii kuhusu kuja kwa Masihi. Kuja kwa Masihi kulikuwa ni tumaini kuu, si kwa Yuda peke yake, bali kwa ulimwengu wote.

Mojawapo ya ujumbe wa aina hii uko katika sura ya ishirini na tisa. Watu walikuwa karibu kuingia katika hali ya utumwa huko Babeli. Kupitia barua kutoka kwa Yeremia, Mungu aliwaambia: *'Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema Bwana, ni mawazo ya amani, wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho. Nanyi mtaniita, mtakwenda na kuniomba, nami nitawasikiliza. Nanyi mtanitafuta, na kuniona, mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote. Nami nitaonekana kwenu, asema Bwana, nami nitawarudisha watu wenu waliofungwa, nami nitawakusanya ninyi, nikiwatoa katika mataifa yote, na katika mahali pote, nilikowafukuza, asema Bwana; nami nitawaleta tena, hata mahali ambapo kutoka hapo naliwafanya mchukuliwe mateka* **(29:11-14)**.'

Huu ni muhtasari wa ujumbe mkuu ambao Yeremia alishiriki na watu wa Yuda walipoanza harakati zao za kuchukuliwa mateka hadi nchi ya utumwa huko Babeli: *'Mungu wenu awapendaye anawaadhibu ninyi, lakini hii ni kwa ajili ya wema wenu, na wala siyo kwa kuumizwa kwenu. Mungu ataka kuwapa ninyi tumaini na tarajio la hapo baadaye. Mkiwa huko Babeli, mwiteni Mungu. Njooni na mfanye maombezi kwake Mungu. Ikiwa mtamtafuta Mungu kwa mioyo yenu yote, Mungu atawasikia nyinyi. Mungu atawapateni ninyi naye atawaleta ninyi kutoka katika nchi ya utumwa hadi mlikotoka.'*

Yeremia alipotabiri kuhusu kutekwa kwao, alikuwa tayari kuteseka na kudhihakiwa kwa ajili ya ujumbe wake. Hata hivyo, aliamini kwamba ujumbe wake ulikuwa umetoka kwa Mungu naye Mungu alikuwa amempa ujumbe wa kweli. Na hivi ndivyo ilivyo kuwa! Jambo la kutilia maanani kuhusu unabii wake Yeremia ni kwamba wote ulipata kutimizwa.

Unaposoma unabii wake Yeremia, tazama ujumbe kuhusu adhabu pamoja na hukumu ya Mungu kwa watu wa Yuda. Hata hivyo, itakuwa bora zaidi ikiwa hautaepuka ujumbe ule wa tumaini. Timiza jumbe zote mbili katika maisha yako, na ukumbuke: Wakati Mungu anapokuadhibu, Yeye anafahamu mipango aliyo nayo kwa ajili yako - mipango ya kukufanikisha kiroho, mipango ya kukupa tumaini na matarajio ya baadaye. Jambo lililo muhimu ni kwako wewe kukumbatia adhabu yake Mungu kwa njia bora, ili mwishowe Mungu aweze kukurudisha kutoka njia zako za upotovu na utumwa na kuwa chombo kipya.

# SURA YA TANO

## 'Mwongozo Wa Utekaji'

Watu wakikaribia kuchukuliwa mateka na kusafirishwa hadi Babeli, Yeremia aliwapa maneno ya tumaini ili waweze kustahimili huko uhamishoni. Wale waliopona kutokana na maafa makubwa wakati Yerusalemu ilipoanguka walikuwa wamehuzunika, wenye hofu kuu pamoja na machukio juu ya yale yaliyokuwa yametokea. Maneno haya kutoka kwa Yeremia yangewasaidia kuweza kustahimili miaka hiyo sabini huko uhamishoni: *'Bwana asema hivi, Mwenye hekima asijisifu kwa sababu ya hekima yake, wala mwenye nguvu asijisifu kwa sababu ya nguvu zake, wala tajiri asijisifu kwa sababu ya utajiri wake; bali ajisifuye na ajisifu kwa sababu hii, ya kwamba ananifahamu mimi, na kunijua, ya kuwa mimi ni Bwana, nitendaye wema, na hukumu, na haki, katika nchi; maana mimi napendezwa na mambo hayo, asema Bwana* **( Yeremia 9:23-24)**.

Neno lingine ambalo hutumiwa kwa kujisifu katika tafsiri nyingine ni 'kujitukuza' Yeremia alikuwa akisema kwa uhakika kuwa, *'Ikiwa wewe u tajiri, usijitukuze katika utajiri wako. Ikiwa wewe una uwezo, usijitukuze kwa sababu ya uwezo wako. Na ikiwa wewe una hekima au elimu kuu, usijitukuze kwa hekima au elimu yako kuu.'* Neno 'Utukufu' au 'kujitukuza' linamaanisha, 'kuileta uwezo wote wa hali ye yote yale, ili kuonyesha dhahiri kabisa maana ya Mungu ni nani na ni nini na na anaweza kuwa nini katika maisha yako.'

Katika hali hii, Yeremia analitumia jina hili sio kuhusiana na Mungu, bali kwa mateka waliohamishwa. Kwa mfano, Yeremia anasema kwa mtu tajiri, *'hauwezi kuendelea kutumainia utajiri wako ili kudhihirisha uwezo wako kamili ulio katika maisha yako. Hauwezi kutosheka kutoka na utajiri.' Kati ya mateka watu waliokuwa matajiri walikuwa wamenyang'any'wa utajiri* wao wote. Inawezekana kuna wakati walitukuka katika utajiri wao kabla ya Yerusalemu kutekwa na kuharibiwa, lakini sio kwa wakati huu. Vivyo hivyo, Yeremia alikuwa akiwaambia wenye elimu na uwezo mkuu, kuwa *'mwenye hekima, kwa sasa haujihisi kuna na hekima, je! Unajihisi hivyo, huku ukiwa uhamishoni na umefungwa kwa minyororo? Wewe mwenye nguvu, hauwezi kujitukuza tena kwa ajili ya nguvu zako. Huko Babeli mtalishwa posho lake mfungwa na kuwekwa katika hali ya njaa na kuwa na unyonge mwingi.'*

Kufikia hapo, huu unaonekana kana ni ujumbe usio mzuri. Lakini hapa ndipo palipo na sehemu nzuri ya ujumbe wake Yeremia. Mungu anawaambia mateka wale kwa kupitia Yeremia, *'Ikiwa kwa hakika unataka kufahamu maana na kusudi la maisha na kutosheleza utimilifu wako, basi inakubidi kunijia mimi kwa njia ya kuhusiana na asili yangu na kunifahamu Mimi ni nani.'* Yeremia anahubiri, *'Wewe utatosheleza jinsi ya uwezo wako kikamilifu wakati utakapofahamu maana kamili ya utu wake Mungu humu duniani na juu Mbinguni. Unaweza kufahamu maana ya utu wa Mungu kisha maana ya utu wako kibinafsi ikiwa utafahamu kwamba Mungu hujidhihirisha mwenyewe ulimwenguni kupitia sifa za utu na maana yake.'* Sifa za tabia yake Mungu zinafanya utu na maana yake Mungu.

Haya mahubiri makuu ya Yeremia, anahubiri, *'Hivi ndivyo unaweza kumfahamu Mungu. Mungu anaweza kufahamika kupitia maana ya utu wake. Kupitia upendo wake kamilifu, kupitia haki yake na hukumu yake iliyo haki.'* Basi, maneno haya yaliwapa mambo ya kutafakari huku wakiwa katika kazi ngumu ya utumwa huko Babeli: wao walifahamu kwamba hawatapata utimilifu na kutosheka kutokana na utajiri au elimu au nguvu zao za mwili. Wao walifahamu ni lazima kupata maana na timizo lao mahali pengine. Kulingana na nabii, huu ulikuwa wakati mwema wa kufahamu kusudi na timizo kamilifu la kumfahamu Mungu. Hiki ndicho kitu ambacho Mabwana zao watekaji hawangeweza kuchukua kutoka kwao.

**Thibitisho La Kurudi Kwao**

Katika kitabu cha Yeremia **32-33,** tunasoma kuhusu jambo moja jema ambalo Yeremia alitenda. Hii ni katika kilele cha uvamizi na utekaji, mwisho wa uongozi wake Mfalme Zedekia. Mji ulikuwa tayari umeangukia mikono mwa maadui. Huku Yeremia akiwa kifungoni kwa yale aliyokuwa akihubiri, alipokea ufunuo kutoka kwa Mungu. Mungu alimfunulia Yeremia kwamba binamu wake Hanameli angewasili na kumwuliza kulinunua shamba lililokuwa lake huko Anathothi. Huku Yerusalemu ikiwa imezingirwa, haukuwa wakati mwema kununua lile shamba lilokuwa karibu Yerusalemu! Lakini Mungu akamwambia Yeremia kuinunua lile shamba. Kwa hakika, Yule Hanameli aliwasili na kusema, *'Tafadhali ulinunue shamba langu lililoko Anathothi, katika nchi ya Benyamini; maana haki ya urithi ni yako, ujinunulie.'*

Yeremia alikubali kulinunua lile shamba na kufanya jambo hilo kuwa kubwa mno. Akawatafuta mashahidi, wanasheria, waandishi na kufanya ununuzi ule kuwa rasmi na wenye kufahamika kote vyema. Baadaye, yeye aliitwaa ile hati ya kununua, na kuipiga muhuri na kuiweka ndani ya gundulia. Kisha akauhubiri ujumbe mwingine wenye ishara. Haya ndiyo mahubiri yake: *'Mimi nimekuwa nikiwaeleza kwamba ninyi mtarudi kutoka Babeli. Naam, hebu niwaonyeshe kwamba kweli naamini kutakuwa hivyo. Hivi karibuni niliinunua shamba yamkini maili tatu kutoka hapa Yerusalemu. Je! Mnadhani kuwa mimi naweza kulitenda tendo hili ikiwa sina na imani kwamba sisi tutarudi hapa? Mungu atairejesha fanaka yake Israeli' Hakikisha kwamba utasoma ujumbe huo wenye ushawishi na ufasaha mwingi ambao Yeremia aliuhubiri na kufafanua kitendo hiki cha* ***(Sura ya 32).***

Ujumbe huu wenye kuvutia na matumaini katika sura ya thelathini na mbili ndio mazingira ya kihistoria aliyoyahubiri maneno haya yanayofahamika: *'Niite, nami nitakuitikia, nami nitakuonyesha mambo makubwa, magumu usiyoyajua (***Yeremia 33:3**).' Je! Wewe umewahi kumwitia Mungu? Yeye anataka kila mmoja wetu kumwita kwa kuwa Yeye anataka kutuonyesha mambo yaliyo makuu ambayo hatujawahi kuyaona hapo mwanzoni.

Hapa unaweza kuona kwamba mahubiri ya Yeremia hayakuwa yenye kutia huzuni tu. Kulikuwepo na tumaini kuu kwa watu wa Mungu katika jumbe zake. Hiyo ndiyo iliyokuwa tumaini yao watu wa Yuda wakati walipokuwa wakichukuliwa mateka hadi Babeli.

**Mambo Ya Moyoni**

Tunapochunguza kwa ufupi jumbe zingine zake Yeremia, kumbuka kwamba hatuna utaratibu wo wote. Yeye pamoja na mwandishi wake Baruku, hawakunakili mahubiri yote alipokuwa akihubiri, bali aliandika jinsi alivyokuwa akikumbuka miaka mingi alipokuwa huko gerezani.

Moja ya muhtasari wa mahubiri ya Yeremia yapatikana hapo mwanzoni mwa kitabu cha Yeremia. Bwana alisema hivi kupitia Yeremia, *'Kwa maana watu wangu wametenda maovu awili; wameniacha mimi, niliye chemichemi ya maji ya uzima, wamejichimbia mabirika, mabirika, yavujayo, yasiyoweza kuweka maji* **(Yeremia 2:13).'**

Watu walikuwa wamegeukia mbali na Mungu pamoja na hekima itokayo katika Neno lake. Waliamini waandishi ambao walifanya sheria ya Mungu kuwa uongo, kulingana na Yeremia. Huyu nabii mkuu anaandika kuwa, 'Mwasemaji, Sisi tuna akili, na torati ya Bwana tunayo pamoja nasi? Lakini, tazama, kalamu yenye uongo ya waandishi imeifanya kuwa uongo **(Yer. 8:8).'** Wakati watu wanapofanikiwa katika kukushawishi kwamba Neno la Mungu haliaminiki, je! Utaamini lipi? Kile ulicho nacho ni hekima na falsafa ya mwanadamu tu. Naye huyu Yeremia aliuliza ni hekima gani iliopo ikilinganishwa na hekima inayopatikana katika Neno lake Mungu?

**Watu Wanaweza Kubadilika?**

Je! Unafahamu Biblia haielezei kwamba ujibadilishe au ujaribu kwa bidii kuwa mwema? Ni jambo la kushangaza sana kuwaona baadhi ya watu ambao hufikiria huu ndio ujumbe mkuu wa Biblia: Jitahidi uwezavyo upate kuwa mwema zaidi. Maandiko hayaelezi hivyo. Kwa kweli, Yeremia anatufanyia mzaha kwa tendo letu la kujaribu kujisaidia wenyewe. Yeye anahubiri, *'Mbona unatanga-tanga hivi upate kugeuza mwendo wako? Wakati chui anapobadilisha madoadoa yake, na wakati ambapo Mkushi atakapoibadilisha rangi ya ngozi yake, hapo ndipo ninyi mliozoea uovu mtakapoanza kutenda yaliyo mema* **(Yer. 2:36).**'

Sisi hatuwezi kujibadilisha wenyewe. Tunahimizwa, *'Bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu. . .* **(Warumi 12:2).'** Yesu anatuambia kwamba ni lazima tuzaliwe mara ya pili. Wakati ambapo sisi tunageuzwa au kuzaliwa kwa mara ya pili, kwetu, huu ni ushuhuda ambao hatutendi lo lote. Hili sio jambo moja na kuambiwa ubadilike, au jitahidi zaidi kuwa mwema.

**Ni Nani Ajuaye Mioyo Yetu?**

Yeremia pia aliona haya kusema kuhusu moyo wake mwanadamu: *'Moyo huwa mdanganyifu kuliko vitu vyote, una ugonjwa wa kufisha; nani awezaye kuujua?* **(Yeremia 17:9)**.' Jibu kwa hakika ni Ni Mungu peke yake awezaye kuijua mioyo yetu. 'Mimi, Bwana, nauchunguza moyo, navijaribu viuno, hata kumpa kila mtu kiasi cha njia zake, kiasi cha matunda ya matendo yake **(Yeremia 17:10).**'

Mungu anafahamu moyo wako. Labda wewe ulidanganya jamii yako, au marafiki zako au hata labda wewe mwenyewe, lakini huwezi kumdanganya Mungu. Yeye anafahamu moyo wako naye anataka kuufanya kuwa mpya. Omba jinsi Daudi mwenye hekima alivyo omba: *'Ee Mungu, unichunguze, uujue moyo wangu, Unijaribu, uyajue mawazo yangu; Uone kama iko njia iletayo majuto ndani nyangu; Ukaniongoze katika njia ya milele* **(Zaburi 139: 23-24).'**

Kote katika kitabu cha Yeremia, tunahitaji kutazama mambo tunayohitajika kutenda kutokana na jumbe hizo kuu za huyu nabii. Kuna wakati ambapo Mungu anahitaji kutuadhibu na kutubadilisha kuwa vyombo vipya. Wakati matokeo ya dhambi zetu hayawezi kubadilishwa na makofu yake, tunahitaji kufanyika kuwa vyombo vipya jinsi ilivyo katika jumbe zake Yeremia alizohubiri wakati Mungu alipomtuma katika jumba la mfinyanzi.

# SURA YA SITA

## ‘Habari Za Huzuni Za Mungu’

Yeremia alikuwa na maono ya vikapu viwili vya tini **(Sura ya 24).** Baadhi ya tini zilikuwa nzuri na zenye kuiva, ilhali zingine zilikuwa zimeharibika na kuoza. Naye Bwana akamwambia Yeremia, *‘Tini zilizo nzuri ndivyo nitakavyowaangalia mateka wa Yuda, niliowatoa katika mahali hapa, waende mpata nchi ya Wakaldayo, wapate mema, nami nitawaingiza katika nchi hi tena; nami nitawajenga, wala sitawabomoa; nitawapanda wala sitawang’oa. Nami nitawapa moyo, wanijue ya kuwa mimi ni Bwana; nao watakuwa watu wangu, nami nitakyuwa Mugnu wao; kwa maana watanirudia kwa moyo wao wote.’*

*‘Na habari za tini zile mbovu, sizisoweza kuliwa, kwa kuwa ni mbovu sana; hakika, asema Bwana, ndivyo nitakavyomtoa Sedekia, mfalme wa Yuda, na wakuu wake, na mabaki ya Yerusalemu, waliosalia katika nchi hii, na hao wanaokaa katika nchi ya Misri. Naam, nitawatoa watupwe huko na huko katika falme zote za dunia, wapate mabaya; wawe kitu cha kulaumiwa, na mithali, na dhihaka, na laana, katika mahali pote nitakapowafukuza. Nami nitatuma upanga, na njaa na tauni, kati yao, hata watakapopotelea mbali katika nchi niliyowapa, wao na baba zao.’*

Yeremia aliuhubiri ujumbe huu wakati wote. Kulikuwa na aina mbili ya watu huko Yerusalemu wakati mji ule ulipokuwa ukianguka mikononi mwa milki ya Babeli - Wale ambao walitambua kuchukuliwa kwao hadi Babeli kulikuwa ni adhabu kutoka kwa Mungu, wao walisafiri hadi Babeli, na kuipokea adhabu ile pamoja na kufanya toba. Na wale kama Zedekia, waliokataa kutambua tukio lile kama tendo lake Mungu, wao walikataa mahubiri yake Yeremia, na kuasi kinyume cha Babeli. Wao walifanyika kuwa kama tini zenye kuoza na kuharibika au gundulia lile lililovunjwa na Yeremia.

**Hoja Kinyume Cha Utu Wa Kibinadamu**

Baadhi ya mahubiri ya Yeremia yanajulikana leo kama ‘utu wa kibinadamu.’ Baadhi ya dhana nyingi za kielemu ambazo ni maarufu siku zetu, ambao tunazichukulia kuwa za kisasa, wakati mwingi huwa ni elimu mpya bali ni zile za kale. Dhana hizo huwa ni mafunzo ya zamani yenye upotovu yaliyoibuka upya. Sawa na elimu hii, dhana hizi ambazo hufundisha kwamba mwanadamu hahitaji Mungu ila mwanadamu peke yake anatosha, zinapatikana katika historia ya kale. *‘Mimi ndimi Bwana wa maisha yangu na nahodha wa moyo wangu,’* Hili ndilo ungamo kuu la wafuasi wa elimu hii. Lakini tunapoendelea kujifunza maisha ya watu kama Musa, tunaona elimu iliyo kinyume na dhana hii. Tunapata kweli timilifu za kiroho zitokazo katika maisha yao, kama, ‘Mimi siye, Ila Mungu ndiye, na yupo pamoja nami. Mimi siwezi, bali Yeye anaweza, naye Yupo pamoja nami.’

**Je! Tunahitaji Mungu?**

Yeremia akumbana na dhana za wenye elimu ya utu wakati anapohubiri ujumbe sawa na ule ulio katika sura ya kumi: *‘Ee Bwana, najua ya kuwa njia ya mwanadamu haimo katika nafsi yake; kuelekeza hatua zake si katika uwezo wa mwanadamu* ***(23)****.’ Hebu tilia maanani kuwa, ‘Amelaaniwa yule anayemtumainia mwanadamu, yule anayetegemea mwili kwa ajili ya nguvu zake na ambaye moyo wake wageukia mbali na Bwana.’ Kisha Yeremia atupatia matokeo bora kutokana na kweli ile: ‘Amebarikiwa mtu ambaye anamtegemea Bwana, na ambaye ujasiri wake umo ndani Yake (***7***).’*

Watu wengi huamini kuwa hawahitaji mchungaji. Wao hawajawahi kuwa na shida ye yote ambayo hawawezi kuitatua wenyewe. Wao huamini akili yake binadamu, na ubunifu wake pamoja na vipawa vyake vinatosha. Lakini Maandiko yanazidi kusema, *‘La, Hasha! Hayo hayatoshi. Wewe unahitaji mchungaji. Unahitaji hekima kutoka kwa Mungu, na pia unahitaji uweza mkuu (neema) kutoka kwake Mungu ili kutumia hekima unayopokea kutoka Kwake* **(Yakobo 1:5; 2Wakorintho 9:8).** Haya ndiyo mafundisho sahihi yenye kufundishwa na manabii wote, kote katika Agano la Kale na Jipya.

**Tayari Kwa Neno**

Tiba yake Yeremia kwa kuasi kwa Yuda, na dhambi ambayo ilileta uhamisho hadi Babeli, imedhihirishwa katika ujumbe mwingine mkuu unaopatikana katika sura ya nne: *'Maana Bwana awaambia hivi watu wa Yuda na Yerusalemu; Ulimeni udongo katika konde zenu, wala msipande mbegu kati ya miiba. Jitahirini kwa Bwana, mkaziondoe govi za mioyo yenu, enyi watu wa Yuda na wenyeji wa Yerusalemu; ghadhabu yangu isije ikatoka kama moto, ikawaka hata mtu asiweze kuizima, kwa sababu ya uovu wa matendo yenu* **(3,4).**'

Ujumbe huu wa kuvutia wa Yeremia ni sawa na ule wa Bwana unaopatikana katika vitabu vya Injili, ambao unatajwa kama, 'hadithi ya mpanzi.' Yesu alisema wakati Neno la Mungu linahubiriwa, ni kama mkulima akipanda mbegu. Wakati mkulima anapanda mbegu, huwa zinaanguka mahali mbali mbali ya udongo.

Aina hizo nne za udongo ni mfano wa tofauti ambazo watu hulipokea Neno wakati linapohubiriwa: *'Wakati mwingine Neno halipenyi katika mapenzi yake msikilizaji; ilhali wakati mwingine, Neno halipenyi katika nia na mawazo yake, lakini linapoanza kukua linasongwa kabisa na kwekwe ambazo zinawakilisha fedheha za ulimwengu huu, mali na mambo mengine yenye kupotosha; na wakati mwingine hili hukua na kuzaa aina mbali mbali ya matunda.'*

Katika hadithi hii ya kuvutia, inawezekana Yesu alikuwa akijenga juu ya ujumbe wa Yeremia. Nabii aliwaambia watu, *'Maisha yenu ni kama udongo ambao haujalimwa. Na hakuna mbegu iliyopandwa mle kwa muda mrefu mno.'* Wao walikuwa wamesahau kuhusu Neno lake Mungu. Shida za hawa watu pamoja na mazingira yaliyokuwa katika maisha yao, yalikuwa matayarisho kwa udongo wa maisha yao ili kuipokea mbegu ya Neno la Mungu kwa mara nyingine. Mungu alikuwa akiutayarisha udongo wa maisha yao ili kulisikiliza Neno Lake.

Yeremia alizungumzia kuhusu kutahirishwa katika mioyo. Mtume Paulo ambaye pia alitumia usemi huo wa Yeremia, inaonekana alijifunza usemi huo kutoka kwa Yeremia. Paulo aliandika tohara ilikuwa kwa watu wa Agano la kale jinsi ubatizo ulivyo katika Agano Jipya Tohara ilikuwa agizo, sakramenti kwa watu wa Kiyahudi walivyokiri imani yao. Ubatizo ndio njia ambayo Yesu alitufundisha kukiri imani yetu kwake siku hizi.

Agizo lo lote linaweza kufanyika kuwa desturi isiyo na maana. Sherehe ye yote ikiwa haina ukweli wa kile inachowakilisha inaweza kuwa haina maana na kukosa faida. Yesu na mitume, pamoja na manabii walitilia mkazo utofauti wa kukiri na kutenda. Kutenda kwako au jinsi unavyoishi, ni muhimu wakati wote kuliko kukiri kwako, au maneno yale unayosema. Uishi maisha yako ya kila siku kulingana na maagizo ni kuwakilisha kile ambacho Yeremia na Paulo walichotaja kama 'tohara ya moyo.'

Je! Wewe unakiri una imani? Ikiwa ni hivyo, basi usiwe mtu wa kukiri tu, bali ishi kulingana na kile unachokiri.

**Habari Za Mungu Za Kuhuzunisha**

Katika sura ya ishirini na tatu, Yeremia alidhihirisha ucheshi pamoja na dhihaka katika mahubiri yake, kama vile tafsiri ya kifungu hiki inavyoonyesha: *'Mmoja wa watu wao au mmoja wa manabii wao au kuhani atakuuliza, 'Naam, habari za Yeremia zenye kuhuzunisha siku ya leo ni zipi?' Nawe utajibu hivi, 'Habari zipi za kuhuzunisha? Wewe ndiwe habari za kuhuzunisha, kwa kuwa Bwana amekutupilia mbali.' Ilhali kwake yule nabii wa uongo na kuhani pamoja na watu wale wanao dhihaki kuhusu habari za kuhuzunisha za siku ya leo kutoka kwa Mungu, Mimi nitawaadhibu wao pamoja na jamii zao kwa kusema usemi huu.'*

Watu walikuwa wakimdhihaki Yeremia kuwa hakuwa na jambo jema la kusema. Ujumbe wake, jinsi tumeuona, ulikuwa kinyume kwa kuwa uharibifu ulikuwa ukiwajia. Na yale yote

aliyosema yalikuja kutokea, huzuni na ghadhabu, pamoja na tumaini. Mahubiri yake Yeremia yalikuwa ndio tumaini kwa Wayahudi wale waliosikiza jumbe zake pamoja na unabii wa Kimasihi uliochanganyikana na ahadi yake kwao ya kurudi kutoka utumwani. Hii inawakilisha tazamio la tumaini letu kuu siku ya leo la kurudi kwake kwa pili.

**Mzigo Wa Yeremia**

Ujumbe wake ulikuwa wenye shauku kuu: *'Mtima wangu, mtima wangu! Naumwa katika moyo wangu wa ndani; moyo wangu umefadhaika ndani yangu; siwezi kunyamaza; kwa sababu umesikia, Ee nafsi yangu, sauti ya tarumbeta, mshindo wa vita. Uangamivu baada ya uangamivu umetangazwa; kwa maana nchi yote imeharibika* **(Yeremia 4:19-20)**.' Katika ufunuo wa unabii kuhusu utekaji kutoka Babeli, Yeremia kwa hakika alisikia kelele kutoka kwa majeshi ya Babeli pamoja na kilio cha watu wa Yuda. Kwa sababu yeye anaendelea kuwa na ushuhuda wa tisho kuu la matukio yale, anauliza hivi, *'Niione bendera hata lini, na kuisikia sauti ya tarumbeta?* ***(21).*** *' Naye Mungu anamjibu, 'Hadi wakati watu wangu watakapouacha upumbavu wao, kwa kuwa wao hukataa kunisikiza mimi.' 'Wao ni wapumbavu na wenye kupungukiwa na akili wala hawana ufahamu; ni wenye akili katika kutenda mabaya, bali katika kutenda mema hawana maarifa* **(22).'**

Ujumbe huu wa Yeremia unaweza kupokelewa katika kizazi chetu . Sisi tu watu stadi wenye usanifu mkuu katika kuziunda silaha zenye uharibifu mkuu siku ya leo, lakini je! Sisi tunafahamu lililo nzuri? Vita na uhalifu ni mpurukutiko mkuu katika ulimwengu wetu. Sisi tuna akili kuu kuzijenga zana na silaha za Nuclear yaani tonaradi, Kemia na Biolojia kwa ajili ya uharibifu mkuu, lakini hata hivyo, hatuna hata talanta kidogo ya kutenda yaliyo mema. Hata hivyo, hatufahamu kutenda mema ni jambo gani.

**Uvumilivu Wa Yeremia**

Yeremia alielezea tafsiri ya kwanza ya kitabu hiki kwa mwandishi wake mwaminifu Baruku kuanzia katika kisima alipokuwa amefungiwa. Baada ya kumalizia chuo kwa jumbe zake jinsi alivyokuwa akikumbuka, aliuliza kama chuo kile chote kinaweza kusomwa kwa watu katika sikukuu yao ya kufunga kula na kunywa. Jambo hili liliwagusa watu mioyo hivi kwamba baadaye, mfalme alipata kusomewa chuo chote. Huku mfalme akisomewa chuo kile akiwa kando ya moto mkubwa alichukua kila sehemu ya chuo hicho na kukipasua kwa kisu kisha akakitupa kwenye moto kikateketea.

Wakati Yeremia alipo fahamishwa kuhusu jambo hilo, alimtuma Baruku mwandishi wake mwaminifu kutafuta chuo kingine kikubwa zaidi kwa kuwa alikuwa akiandika kitabu hicho kwa mara nyingine. Alikuwa amekumbuka baadhi ya jumbe zingine ambazo hazikuwemo katika chuo cha kwanza. Hivyo basi, alinakili sura hamsini na mbili za chuo au kitabu hicho ambacho tuko nacho hadi wakati huu. Hatungekuwa na kitabu hiki cha Yeremia isipokuwa kwa ajili ya uvumilivu wa nabii huyu mkuu **(Sura 36).**

# SURA YA SABA

## Kitabu Cha Maombolezo

## 'Hata Hivyo, Mungu Anakupenda'

Kitabu cha Maombolezo ni sehemu inayofuatia kitabu cha Yeremia. Katika sura ya hamsini na mbili, Yeremia anaomboleza kwa ajili ya ufunuo wa unabii ambao Mungu alimpa kuhusu utekaji nyara kutoka Babeli. Kitabu cha Yeremia kinamalizika hali nabii yu ngali katika nchi ya Yuda baada ya watu wengi kuchukuliwa na kufanywa watumwa. Kulingana na historia,

inaonekana kwamba alihamia nchi ya Misri na alipata kuuawa huko. Wasomi husema kwamba hatimaye Yeremia alikwenda huko Babeli kuwahubiria watu wa Yuda ambao alikuwa amewapenda sana, ilhali wengine hufikiria aliishi huko Yuda siku zake za mwisho.

Kitabu cha Maombolezo kinalingana na yaliyomo ndani yake 'Nabii mwenye kilio' angali bado analia kwa kuwa nchi ilikuwa imechukuliwa na wavamizi, watu ambao aliwapenda sana; kwani baadhi yao hawakuwa wameangamizwa wakati walichukuliwa mateka katika nchi ya mbali.

Shida moja ambayo anazungumzia katika Maombolezo, ambayo pia ilipata kuzungumziwa na manabii wengine kama Ezekieli na Danieli, ilikuwa kweli wao hawangekuwa karibu na Hekalu. Wayahudi walikuwa wakiamini katika Hekalu, ndipo uwepo wake Mungu ulipok. Na uwepo wake wa Kiuungu uliketi katika patakatifu pa patakatifu ndani ya Hekalu lililokuwa huko Yerusalemu. Kuna njia ambayo kwa hakika Mungu alikuwa akiishi katika Hekalu hasa kwa hawa manabii. Hii ndio sababu nabii Danieli aliuelekeza uso wake hadi Yerusalemu wakati wote alipokuwa akifanya maombi. Mungu alikuwa wapi, kwa watu wake ambao walikuwa wakiishi huko Babeli? Kwa hakika, Yerusalemu ulikuwa ndio mji wake Mungu , nao walijihisi kutenganishwa na mji wao mtakatifu pamoja na Mungu wao mtakatifu.

**Pango Lake Yeremia**

Yeremia aliandika kitabu cha Maombolezo akiwa ndani ya pango juu ya mlima. Mahali hapo hata siku ya leo paitwa 'Pango la Yeremia', na katika mlima uitwao 'Golgotha.' Kwa mapenzi yake Mungu, pango lake Yeremia, lilikuwa juu ya mlima Kaivali, ambapo Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu. Tutaona umuhimu wa tukio hilo la Kiungu hapo tutakapojitosa katika ujumbe wa Maombolezo.

**Utunzi Wa Maombolezo**

Kama mojawapo ya uandishi, Maombolezo ni shairi la hali ya juu, lenye tenzi tano au shairi katika sura zake tano. Kila sura ni shairi tenzi tofauti, na nne kati yake ni zile tenzi zenye mfumo wa kulingana na herufi. Katika shairi hizi zinazolingana na herufi, tenzi ya kwanza hulingana na herufi ya kwanza ilhali ya pili hulingana na tenzi ya pili na kuendelea hivyo hadi kumalizia. Pamoja na urembo wa umbo na mfumo wa lugha yake katika hali ya uandishi, ni ujumbe ulio na uvuvio ambao unafanya kitabu hiki kuwa na nafasi katika Neno lake Mungu.

Ujumbe huu uliovuviwa unagusia janga kuu la kutekwa na uvamizi wa Babeli. Ujumbe huu unaelezwa kwa njia dhahiri, shauku na hisia nyingi mno: 'Ni kushuhudie nini? Nikufananishe na nini, Ee binti Yerusalemu? Nikusawazishe na nini, nipate kukufariji, Ee bikira binti Sayuni? Kwa maana uvunjifu wako ni mkuu kama bahari, Ni nani awezaye kukuponya? **(Maombolezo 2:13).'** Maelezo yake Yeremia kuhusu uharibifu wa Yerusalemu baada ya uvamizi wa Babeli kwa hakika ni yakuonyesha hofu ambayo ilitokea wakati mji ulipovamiwa na kutekwa na utawala kwa mfano wa Babeli.

Huku tukifikiria kitabu hiki kina huzuni na kukatisha tamaa, Yeremia anatushangaza kwa unabii wa kuvutia mno wa Kimasihi na wenye tumaini. Unaweza kukumbuka pia Ayubu alitenda jambo hilo hilo katika kilele cha dhiki yake. **(Ayubu 19: 25-26).** Katika sura ya tatu ya Maombolezo, akiwa kwenye tundu la kukata tamaa, Yeremia anapokea ufunuo wa unabii wenye kushangaza: *'Ni huruma za Bwana kwamba hatuangamii, Kwa kuwa rehema zake hazikomi. Ni mpya kila asubuhi; Uaminifu wako ni mkuu. Bwana ndiye fungu langu, husema nafsi yangu, Kwa hiyo nitamtumaini yeye. Bwana ni mwema kwa hao wamngojeao, kwa hiyo nafsi imtafutayo. Ni vema mtu autarajie wokovu wa Bwana na kumngojea kwa utulivu* **(22-26).'**

Ujumbe wa tumaini uliofunuliwa Yeremia ulikuwa huu: Mungu haachi kutupenda sisi! Wakati tunapotenda dhambi, hata hivyo, Yeye angali anatupenda. Tumaini letu lipo katika pendo lake Mungu. Yeremia aliwaambia wale mateka walipokuwa wakihamishwa hadi Babeli, *'Msijitukuze kwa ajili ya utajiri wenu, nguvu zenu, hekima yenu au labda elimu yenu. Jitukuzeni katika Mungu. Ni lazima umfahamu Mungu na upate kutosheka na utimilifu wako kutoka kwake. Na unaweza kumfahamu Mungu kwa kuweka imani yako kwa pendo lake ambalo halina masharti wala haliwezi kumalizika pamoja na rehema yake.'* Mungu hapa anamfanya Yeremia kufahamu, hatuwezi kupata

pendo lake kwa matendo yetu mema au hatuwezi kupoteza upendo wake kwa sababu ya matendo yetu maovu. Mungu haachi, wala hataacha kutupenda.

**Thibitisho La UPendo Wa Mungu**

Katika Sura ya tatu ya Maombolezo, pia tunasoma, *'Ni nani asemaye neno nalo likafanyika, Ikiwa Bwana hakuliagiza? Je! Katika kinywa chake Aliye juu Hayatoki maovu na mema? Mbona anung'unika mwanadamu aliye hai, Mtu akiadhibiwa kwa dhambi zake? Na tuchunguze njia zetu na kuzijaribu, Na kumrudia Bwana tena* **(37-40).'**

Jinsi Yeremia anavyoeleza tumaini kuu, yeye anashiriki ukweli ambao tuliugundua katika kitabu cha Ayubu nyakati njema na zilizo ngumu hutoka kwa Mungu **(Ayubu 2:10)**. Kweli hii pia inafundishwa na Sulemani, ambaye alihubiri kwamba tunahitaji kufurahia wakati tunaishi katika fanaka. Lakini katika nyakati za maovu, tunahitaji kutambua Mungu ndiye aliyefanya nyakati hizo. Yeye anaanza mafunzo haya kwa kutuambia, ni heri kuiendea nyumba ya matanga, kuliko kuiendea nyumba ya karamu. Kwa maana huo ndio mwisho wa wanadamu wote, naye aliye hai atautia moyoni mwake. Siku ya kufanikiwa ufurahi, na siku ya mabaya ufikiri **(Mhubiri 7:2,14).'**

Unaweza kukumbuka watu wa Mungu waliweza kuabukizwa ugonjwa usio na tiba kwa sababu ya kuabudu sanamu. Dhambi yao ya kuabudu sanamu haikuwa na kifani, na hii iliwahusisha kuhani walaghai na wale manabii wa uongo. Lakini ujumbe wake Yeremia na wa manabii waliokuwa uhamishoni huko Babeli ulikuwa na tumaini hili: *Mungu anakupenda sana hivi kwamba hangelipenda kukuona katika hali ya kupotea siku baada ya nyingine, hasa baada ya kuishi katika dhambi. Mungu hataruhusu hayo kutokea kwenu kwa kuwa ninyi ni watu wake.'*

Funzo kwetu ni kwamba, Mungu huturudi kwa ajili ya dhambi zetu, na adhabu ile huwa thibitisho, sisi tu wana wake Mungu. Na kama wazazi, tunahitajika kuwarudi watoto wetu ikiwa tutaona wakitenda kosa. Nasi hatuwezi kuwarudi watoto wa majirani zetu, kwa wao sio wetu. Mwandishi wa kitabu cha Waebrania anaandika kuwa, 'maana yeye ambaye Bwana ampenda, umrudi, Naye humpiga kila mwana amkubaliye **(Waebrania 12**).'

# SURA YA NANE

## Unabii Wake Ezekieli

## 'Mambo Yote Ya Kuogofya Na Ya Ajabu'

Watu wa Mungu walipokuwa wakisafirishwa hadi uhamishoni Babeli, yule mwandishi wa Zaburi alisema kwamba watesi wao waliwadhihaki. *'Tuimbieni baadhi ya nyimbo za Sayuni!'* Mwandishi huyu anazidi kusema, *'Tuuimbeje wimbo wa Bwana Katika nchi ya ugeni?* **(Zaburi 137:4)**

Haya ndiyo mazingira ya kihistoria nabii Ezekieli na Danieli walipata kuishi maisha yasiyo ya kawaida na kupata kuhudumu kama manabii. Ezekieli na Danieli walikuwa wa rika moja. Danieli alichukuliwa mateka hadi Babeli akiwa na umri wa miaka kumi na minne. Naye Ezekieli alichukuliwa mateka hadi Babeli miaka tisa baadaye wakati alikuwa na umri wa miaka ishirini na tano. Yeye alihubiri katika kambi za watumwa, alikuwa nabii wa pekee kuwahi kuhudumia watumwa moja kwa moja bila kizuizi cho chote.

Mungu hakutaka watu wake, ingawa walikuwa uhamishoni kukosa nabii. Hivyo, Yeye alimwagiza kijana Ezekieli kwenda uhamishoni na kuwahudumia mateka. Msitari wenye ufunguo katika kitabu hiki ni: *'Nami nikatafuta mtu miongoni mwao, atakayelitengeneza boma, na kusimama mbele zangu mahali palipobomoka, kwa ajili ya nchi, nisije nikaiharibu, lakini sikuona mtu* ***(Ezekieli 22:30).'*** *Mungu alimtaka mtu miongoni mwa mateka wale, ambaye 'angelisimama mahali palipobomoka'* kati ya Mungu na watu wake. Naye alimpa Ezekieli agizo kuwa ndiye atakuwa mtu yule.

**Maandiko Yenye Ufunuo Wa Mambo Ya Nyakati Za Mwisho**

'Mambo Yote Ya Kuogofya na Ya Ajabu' ni kichwa mwafaka cha kitabu cha Ezekieli kwa kuwa kimejaa baadhi ya mambo ya kuogofya na unabii wa ajabu. Kuna hali ambayo huyu Ezekieli mwenyewe alikuwa ni nabii wa kuogofya na wa ajabu. Ukiwalinganisha manabii, unaweza kumwona Danieli, Ezekieli na mtume Yohana kuwa walikuwa uhamishoni wakati walipoandika vitabu vya Danieli, Ezekieli na Ufunuo. Danieli na Ezekieli walikuwa uhamishoni katika nchi ya Babeli ilhali Yohana alikuwa amehamishwa na Warumi hadi kisiwa cha Patimo. Hawa wote watatu waliandika vitabu vinavyotajwa kuwa ni 'maandiko yenye ufunuo wa mambo ya nyakati za mwisho.' Maana yake pia ni 'kuvuta pazia nyuma' ili kwamba watu wapate kuona mambo ambayo labda hawangeyaona kwa njia ye yote.

Maandiko haya yenye ufunuo hayatupeleki tu hadi kwenye pazia, bali pia hutupeleka hadi katika hali ijayo. Nabii wa mambo yajayo hutuonyesha yale yatakayotokea wakati Mungu atakapomaliza historia ya wanadamu kulingana na mpango wake. Wasomi hutaja mpango huu wake Mungu wa kuifunga historia ya mwanadamu kama itikadi ya mambo yajayo.

**Utaratibu Wa Kitabu Cha Ezekieli**

Unabii wa Ezekieli ambao kwa hakika una mpangilio mwema, mpangilio na utaratibu wake upo hivi: Ezekieli anatoa unabii kuhusu uharibifu wa Yerusalemu. Na kama nabii aliyekuwa uhamishoni, sehemu ya lengo la huduma yake ilikuwa ni kukumbana na jumbe za manabii wa uongo, ambao walihubiri kwamba kutakuwa na kurudi kwa mapema kutoka uhamishoni kwa kuwa haya ndiyo mateka walitaka kusikia.

Yeremia anamtaja nabii mmoja wa uongo kwa jina Hanania, ambaye alikuwa mpinzani wake kwamba alisema utumwa hautakuwa wa miaka sabini ila miaka miwili peke yake. Yeremia alikumbana naye na kumtabiria kwamba yeye Hanania angelikufa kabla ya mwaka kupita. Unabii huu wa Yeremia ulitimia kama alivyotabiri **(Yeremia 28:11-17).** Hata hivyo, inaonekana walikuwepo manabii wengi wa uongo waliouhubiri ujumbe huu.

Katika sura za kwanza ishirini na nne za kitabu chake, Ezekieli anapinga unabii huu wa uongo na kutilia mkazo kweli kwamba Yerusalemu itaharibiwa. Kama alivyokuwa Yeremia, Ezekieli pia alihubiri kwamba hapakuwa na njia ye yote ya kuepukana na uvamizi kutoka Babeli pamoja na uharibifu wa Yerusalemu.

Katika ya sura ishirini na tano hadi thelathini na mbili, Ezekieli alitabiri kinyume cha Babeli, taifa ambalo lingeharibu Yerusalemu. Yeye alifuatia unabii huu wenye matumaini - kwamba Yerusalemu ingeinuka tena na kuundwa upya **(Sura 33-40)** Sura nane zinazomalizia kitabu cha Ezekieli zina unabii wa mambo ya baada ya ya siku za mwisho. Alitabiri kwamba mahali pale ambapo Hekalu la Sulemani liliposimama, patajengwa Hekalu lingine la milele.

**Agizo La Ezekieli**

Mahubiri mengi ya Ezekieli yalimjia kwa njia ya maono ambayo mengi yaliweza kupatikana katika kitabu cha Ufunuo. Ufunuo wa Ezekieli wa kwanza unaanza hivi: 'Nikaona, na tazama, upepo wa dhoruba ulitoka upande wa kaskazini, wingu kubwa sana, pamoja na moto, ukifanya duara ya nuru, na mwangaza pande zote, na katikati yake kitu kama rangi ya kaharabu, katikati yake mfano wa viumbe hai vinne. Kuonekana kwao kulikuwa hivi; *walikuwa na sura ya mwanadamu. Na kila mmoja alikuwa na nyuso nne, na kila mmoja alikuwa na mabawa manne. . . Kwa habari za mfano wa nyuso zao; walikuwa na uso wa mwanadamu; na hao wanne walikuwa na uso wa simba upande wa kuume; na hao wanne walikuwa na uso wa ng'ombe upande wa kushoto; na hao wanne walikuwa na uso wa tai pia. . . Basi, nilipokuwa nikivitazama vile viumbe hai, tazama, gurudumu moja juu ya nchi, karibu na kila kimoja cha vile viumbe hai, pande zake zote nne. . .Walipokwenda hao, yalikwenda*

*hayo nayo; na waliposimama hao, yalisimama hayo nayo; na walipoinuliwa hao juu ya nchi, magurudumu yaliinuliwa karibu nao; maana roho ya viumbe hai ilikuwa ndani ya magurudumu* **(Ezekieli 1:4, 10, 15, 21).'**

Viumbe hawa wanne ni sehemu muhimu ya maono hayo. Mtume Yohana pia aliwataja hawa viumbe katika kitabu cha Ufunuo, wakati mlango ulipofunguliwa huko mbinguni katika maono yake ya mbinguni. Katikati ya kiti cha Enzi aliona hawa viumbe wanne walikuwa ni wale wale. Wa kwanza alikuwa ni kama simba, wa pili alikuwa ni kama fahali au ng'ombe, naye wa tatu alikuwa ni kama mtu, ilhali yule wa nne alikuwa ni kama tai **(Ufunuo 4:6,7).**

Wasomi wengi wanaamini maono haya wanayoshiriki katika kitabu cha Ezekieli na Yohana ni muhtasari wa ufunuo wake Mungu katika Maandiko. Wakati Mungu alipojidhihirisha kwa mara ya kwanza juu ya mlima Sinai, Yeye alinguruma kama simba. Njia nyingine ambayo Mungu alijidhihirisha kwa mwanadamu ilikuwa kwa njia ya mfumo ule mkuu wa dhabihu unaoelezwa katika kitabu cha Kutoka na Mambo ya Walawi. Yule fahali au ng'ombe anawakilisha wanyama ambao walitolewa dhabihu kwa ajili ya dhambi za wanadamu.

Mwandamu aliye kati ya hawa viumbe wanne anatupeleka hadi katika Injili, pale Mungu anafanyika kuwa mwanadamu. Mungu aliishi kati yetu kwa miaka thelathini na mitatu. Wengi husema huyu tai anawakilisha Mungu. Naye mtu huyu aliyepata kuishi kati yetu, alikuwa 'ni mwanadamu kamili na Mungu kamili ' jinsi ambavyo ungamo linenavyo. Kufanyika mwili kwake Yesu Kristo kulikuwa ndio kilele cha ufunuo wake Mungu katika ulimwengu huu.

Magurudumu yanaweza kuwakilisha ufunuo unaoendelea wa Mungu ambao yamkini unawahusisha manabii waliohusika katika kutangaza ufunuo ule, kwa kuwa roho wa viumbe wale alikuwa kwenye magurudumu yale. Hizo ni baadhi ya tafsiri zinazoweza kutumika katika maono yake Ezekieli ya kwanza.

Ezekieli alipata mwito wa Agizo lake kutoka kwa Mungu **(sura ya 2)**, baada ya kuona maono yale. Hii inaweza kutajwa kama 'ushuhuda wa kuja kwake' Ezekieli. Je! Unaweza kukumbuka kuja kwake Isaya? Manabii na watu wote wakuu wake Mungu katika Agano la Kale walikuwa na ushuhuda wa kule kuja na kwenda kwao. Ushuhuda fulani maishani mwao uliwaleta kwake Mungu na pia walikuwa na ushuhuda walipo 'kwenda kwa ajili' yake Mungu.

Manabii pamoja na watu wengine wa Mungu katika Agano la Kale walikuwa na ushuhuda wa kumjia Mungu ambao wakati mwingine ulichukua miaka mingi, kama katika maisha yake Musa. Yeye alikuwa na miaka themanini ya kumjia Mungu na miaka mingine arubaini ya ushuhuda wa kwenda kwa niaba yake Mungu. Hii ndiyo sababu miaka yake ya kwenda ilikuwa yenye uwezo mkuu; miaka hiyo arobaini ilitanguliwa na miaka themanini ya kumjia Mungu.

Katika sura ya kwanza, maono haya makuu ya hawa viumbe wanne na magurudumu yalikuwa ndio ushuhuda wa kumjia Mungu wake Ezekieli. Wakati wa mwito wake Ezekieli, watu wa Yuda walikuwa wamepoteza maono yao ya Mungu. Wao hawakuwa na Yerusalemu, wala Hekalu, pia hawakuwa na Neno lake Mungu wala usaidizi wo wote katika ibada zao. Hivyo basi, kiongozi wao wa kiroho wakati ule - Ezekieli - alihitaji kupata ushuhuda usio wa kawaida wa maono yake Mungu.

Mungu alimpa Ezekieli maono yake mwenyewe kwa njia kadhaa. Kwanza, Ezekieli anasema mara nyingi kwamba, *'Neno lake Mungu likanijia mimi.'* Hii ni kweli kwa manabii wote wa kweli. Ezekieli pia alisema, *'mkono wake Mungu ulikuwa juu yangu.'* Ezekieli anafahamika kama nabii wa Roho Mtakatifu kwa kuwa yeye anamtaja Roho Mtakatifu mara nyingi zaidi ya nabii ye yote. Lakini kile kilichomfanya nabii Ezekieli kuwa na utofauti miongoni mwa manabii, mbingu zilifunguka kwake na kwa hakika uliuona utukufu wake Bwana.

Mungu aliyatoa maono haya yake mwenyewe ili kuwalinda watu wake wasije wakaangamia. Pia, ni maono ambayo Mungu alimpa Ezekieli ili aweze kuhudumu kama nabii nyakati hizo ngumu na mahali penye ugumu - kambi za watumwa huko Babeli.

**Mlinzi Wa Kiroho**

Ujumbe mkuu wa Ezekieli una nakiliwa katika sura ya tatu. Ujumbe huu unaitwa 'Mlinzi wa Nyumba ya Israeli.' Mfano huu misingi yake imo katika desturi itokayo katika miji yenye kuta na ambayo wakati mwingi ilizingiriwa na watekaji wakatili sana. Sulemani pia anatumia mfano wa aina hii wakati anaandika, isipokuwa Bwana aulinde mji yule mlinzi akesha kwa ubatili tu **(Zaburi 127:1)**.' Kulikuwa na walinzi wakati wote wakishika doria juu ya kuta kwenye vinara vyao wakati wa usiku huku wakitazama na kusikiliza kwa ishara na sauti ye yote adui. Mfano wake, Ezekieli shina lake lipo katika wajibu mkuu wa mlinzi kuwaonya raia wake wakati adui anapotokea. Ujumbe wake Ezekieli kuhusu mlinzi unaanza hivi: *'Hata ikawa, mwisho wa siku saba, neno la Bwana, likanijia, kusema, Mwanadamu, nimekuweka kuwa mlinzi wa nyumba ya Israeli; basi, sikia neno hili litokalo katika kinywa changu, ukawape maonyo haya yatokayo kwangu. . . Lakini ukimwonya mtu mbaya, wala yeye hauachi ubaya wake, wala njia yake mbaya, atakufa katika uovu wake; bali wewe umejiokoa roho yako* **(16-17, 19)**.'

Wakati Yeremia aliwakemea manabii wa uongo wa siku zake, alikuwa akisema kwa hakika kuwa, *'Ninyi hamkuwaonya watu kuhusu dhambi zao wala kujaribu kuwaokoa kutokana na uovu wao.' Ezekieli aliendelea kusema, 'Kama nabii, ikiwa wewe utawaonya watu nao wakazidi katika uovu wao, wao watakufa katika uovu wao. Lakini wewe utajiokoa mwenyewe. Bali kama ukishindwa kuwaonya wao, wewe utawajibika kwake Mungu.'*

Mtume Paulo aliamini jambo hili siku zake. Yeye aliandika: *'Kwa maana sisi tu manukato ya Kristo, mbele za Mungu, katika wao wanaookolewa, na katika wao wanaopotea; katika hao wa pili harufu ya mauti iletayo mauti; katika hao wa kwanza harufu ya uzima iletayo uzima. Naye ni nani atoshaye kwa mambo hayo?* **(2 Wakorintho 2:15-16)**.'

Funzo kwetu maishani ni: Ikiwa wewe utashiriki Injili na mtu mwingine na apate kuamini, basi wewe umekuwa manukato yenye harufu ya uzima kwa mtu yule. Lakini ukishiriki na mtu Injili kisha akatae, basi wewe ni harufu ya mauti kwake kwa kuwa umefanya kuwa jambo ngumu kwake kusema kwamba, *'mimi sikufahamu. Mimi sijawahi kukusikia.'* Ikiwa tunaamini Biblia ni Neno la Mungu lililovuviwa, tunahitaji kuungana na Ezekieli kuamini kwamba sisi tu 'walinzi' juu ya roho za wale tunao kutana nao katika maisha yetu.

Hii ndiyo sababu Ezekieli alitilia mkazo kuhusu Roho Mtakatifu katika mahubiri yake. Ezekieli, kama Paulo, alipata utoshelezo na utimilifu wa wajibu wa mkuu katika Roho Mtakatifu. Paulo aliandika: *'Utoshelezo na utimilifu wetu hutoka kwake Mungu.'* Paulo aliamini kwamba wakati yeye aliposhiriki Injili na watu kama Wakorintho, hapakuwa na cho chote kilichotoka kwake, bali kila kitu kilitoka kwa Roho Mtakatifu **(2 Wakorintho 3:5; 1 Wakorintho 2:3-5).** Ni Mungu peke yake awezaye kutufanya watimilifu ili tuwe walinzi wa kiroho.

# SURA YA TISA

## 'Mifupa Mikavu'

Wachungaji wengi ambao wamelihubiri Neno la Mungu maishani mwao yote, wanapenda sana ujumbe mmoja wa Ezekieli aliohubiri katika uwanda ambapo yamkini palikuwa uwanja wa mauaji ya kinyama na katili yaliyofanyiwa watu wengi. Tunasoma Ezekieli aliongozwa hadi bondeni lililojaa mifupa iliyokauka **(Sura ya 37).** Mwito wake Ezekieli kutoka kwa Mungu ulikuwa kwamba akaihubirie ile mifupa.

Kwa lugha ya mafumbo, hii ndiyo changa moto ambayo mchungaji wakati mwingi hukumbana nayo anaposimama mbele ya washirika wake Jumapili. Mhubiri mmoja alisema Kristo atakaporudi, kusanyiko lake litakuwa ndilo la kwanza kufufuliwa kwa kuwa Paulo aliandika

kwamba *'Waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza* **(1 Wathesalonike 4:16).'** Yeye hushangazwa ikiwa ile mifupa inaweza kuishi tena? Je! Mimi ninaweza kuhubiri kwa njia hiyo kwamba Roho Mtakatifu anaweza kuniwezesha pamoja na ujumbe wangu kutiwa nguvu, na uzima wa kiroho kuwaingia hawa watu?

Wakati Ezekieli alipotii maagizo ya Bwana kuhubiria mifupa iliyokauka: *'Akaniambia, Mwanadamu, Je! Mifupa hii yaweza kuishi? Nami nikajibu, Ee Bwana Mungu, wajua wewe. Akaniambia tena, Toa unabii juu ya mifupa hii, uiambie, Enyi mikavu, lisikieni neno la Bwana. Bwana Mungu aiambia mifupa hii maneno haya; Tazama, nitatia pumzi ndani yenu, nanyi mtaishi* **(37:3-5).'**

Watu wa Yuda walikuwa kama mifupa mikavu. Changa moto ambayo Mungu aliweka mbele ya nabii Ezekieli ilikuwa ni, *'Je! Unafikiri kwamba hii mifupa mikavu itapata kuishi tena?'* Katika Maandiko, Mungu wakati wote aliwapa changa moto manabii kuhusu maono yao. Unaweza kutambua kwamba Ezekieli hakusema, *'Ndio, mimi nina imani kwamba yaweza kuishi tena.'* Badala yake, yeye alisema, *'Bwana wewe peke yako wafahamu.'* Nabii hakujitolea mwenyewe kwa Mungu kwa kuwa hakuamini kikamilifu kwamba ile mifupa ingepata kuishi. Naye Mungu akamwambia, *'Ihubirie mifupa!'*

Hapo, Ezekieli akaanza kuihubiria ile mifupa. Baada ya mahubiri mafupi, Ezekieli anasema kulitokea mshindo mkuu; na tazama, tetemeko la nchi, na ile mifupa ikasogeleana, mfupa kwa mfupa. Na baada ya kushikamana pamoja, Ezekieli alipata kuwa na kusanyiko la magofu matupu, bila nyama wala mishipa juu yake. Ezekieli alipewa agizo lingine, 'Hubiri!' Huku akihubiri, mishipa na nyama ilitokea juu yake.

Wakati Ezekieli alipopata jeshi la magofu likiwa na mwili na misuli, yeye angali hakuwa amelijibu swali lake Mungu, *'Kama hii mifupa yaweza kuishi tena?'* Mili hiyo ilikuwa bado ingali maiti. Hapakuwa na pumzi ndani yake. Hivyo basi, agizo likatoka kwake Mungu, *'tabiri, utabirie upepo, mwanadamu...........!'* Katika Biblia, neno hewa, pumzi na roho ni moja. Pumzi hapa ni Roho Mtakatifu. Hii ni kanuni kuu ambayo utaipata kote katika Biblia: Bila Roho Mtakatifu, mhubiri anaitenda kazi ambayo haiwezekani.

Kila nabii wa kweli anafahamu ikiwa Roho Mtakatifu haji kwake na kumwinua juu na pia kuweka mkono wa upako na nguvu, au kumpaka mafuta, kile ambacho anajaribu kufanya hakiwezekani. Wakati Ezekieli alipohubiri kwa Roho Mtakatifu, pumzi iliingia kwenye miili ya maiti hao nao wakawa jeshi kuu.

Funzo kuu la kutekelezwa kwa Wayahudi juu ya yale Ezekieli aliyoagizwa kuhubiri yalikuwa ni: *'Mimi ninaweza na nitawarudisha ninyi kutoka utumwani. Mimi nitawaongoza na pia nataka kuwatoa kutoka Babeli, hadi nchi yenu. Mimi nitaihuisha Isreali na kuifanikisha.'*

Matumizi ya pili ya ujumbe huu mkuu yanatupatia picha ya yanayohusika katika huduma kuu ya kujenga Kanisa siku ya leo. Kuhubiri Injili hulijenga Kanisa. Mifupa ile mikavu inawakilisha wale waliopotea. Kati ya watu takribani bilioni sita siku ya leo, ni wangapi wanaomfahamu Yesu Kristo? Ni wangapi walio na uhai ndani yake Yesu Kristo? Ni wangapi miongoni mwao wanaofahamu maana ya kuwa na Roho Mtakatifu, na pia kuokolewa naye maishani mwao? Yamkini ni wachache mno. Hii ndio changa moto ambayo inakumbana na Kanisa katika siku ya leo. Funzo la kiroho ambalo tunalipokea kutoka katika ujumbe wa Ezekieli kwa mifupa iliyo mikavu ni changa moto hii: Je! Kanisa lake Yesu Kristo linaweza kutiwa nguvu na Roho Mtakatifu hata kutekeleza Agizo Kuu na kuichukua Injili yake Yesu Kristo kwa watu waliopotea ulimwenguni?

Je! Wewe ni mmoja wa mifupa mikavu? Je! Wewe umepotea kwa kuwa haujawahi kusikia au kuamini Injili ya wokovu? Je! Ujumbe huu wahusiana nawe tu kwa sababu waonekana kuwa hai lakini hauna 'Uzima wa kweli?' Je! Wewe unayo pumzi ya Roho wake Mungu katika maisha yako na kwenye huduma yako? Haijalishi mazingira yako yako vipi, labda sio magumu

kama yale Ezekieli aliamkia kila asubuhi. Ikiwa Mungu anaweza kufanya mifupa iliyokufa kuwa hai kwa ajili yake Ezekieli, basi Yeye anaweza kutenda vivyo hivyo kwangu na pia kwako.

Ikiwa Roho anaishi ndani yako, ni kipi unachotenda ili kulijenga Kanisa? Si lazima uwe mhubiri ili kushiriki na watu wengine katika Injili. Ni lazima uamini kwamba Roho wake Mungu atalipaka mafuta Neno Lake unaposhiriki na mtu mwingine. Imesemwa kwamba mwinjilisti ni maskini mwombaji anayemwambia maskini mwenzake pale mkate unapopatikana. Ikiwa wewe ni mmoja wa hao maskini waombaji anayemweleza maskini mwenzake pale mkate upo, tukizungumza kwa kiroho, ni lazima ufahamu uwezo uliopo katika kule kulishiriki Neno pamoja na maombi.

Katika sura ya pili ya kitabu cha Matendo, tunasoma wanafunzi waliishi pamoja katika jamii kuu ya kiroho. Wao walishiriki mali zao na kuumega mkate pamoja - pia walikuwa na mfumo wa maisha wa Ujamaa yaani *socialism*. Mitume walikuwa wasimamizi wa chakula au huduma ya kuwapa watu chakula ambayo iliwafanya kuwa na wakati mwingi katika uandalizi wa chakula hivi kwamba walisahau wajibu wao mkuu wa huduma ya uchungaji. Tunasoma wao walifanya azimio muhimu sana. Waliwachagua mashemasi wa kwanza na kuwaambia, *'Ninyi shughulikieni hii huduma hali sisi tutajitolea wenyewe kwa ajili ya maombi na huduma ya Neno.'* Mungu aliwabariki kwa sababu ya uamuzi wao walipokuwa katika maombi na kulihubiri Neno Lake.

Huu ndio mchanganyiko mkuu ambao Ezekieli alitumia katika huduma yake. Mtu fulani alisema, *'kama tukikutana pamoja, na hakuna anayebadilika, basi hakuna kinachotendeka. Tunapo lihubiri neno, na ikiwa tunapashana habari tu, basi hakuna kile kitakacho tokea kwa hao wasikilizaji. Hata hivyo, ikiwa tutautuafata mfano wake Ezekieli na mitume, tutagundua kwamba wakati maombi yanapotangulia mahubiri yetu, jambo fulani litatokea. Maisha ya watu wasikilizalo Neno yatabadilika milele.'*

Unapotangaza Habari Njema, Mungu anakuwezesha kutangaza wakati 'unapoitabiria mifupa,' na pia kuitabiria pumzi au Roho. Ni lazima umtazame Mungu wakati wote unapohubiri au kushuhudia Injili na mtu mwingine ili upate nguvu ya upako na kuweza maneno yale usemayo. Wakati nguvu zake zinapokutia nguvu pamoja na maneno yako, ile 'mfupa' itapata kuishi tena.

# SURA YA KUMI

## Unabii Wa Danieli

## 'Waaminifu Dhidi Ya Wababeli'

Danieli ndiye nabii wa nne kati ya wanaotajwa kama 'Manabii wakuu' na wa tatu kati ya wale wanaotajwa kama manabii wa utumwani. Tunapo kutana na huyu Danieli - hapo Yerusalemu inapoanguka kwa mara ya kwanza - umri wake ni kama miaka kumi na minne. Hapakuwa na utekaji wa watu wengi wakati huo, isipokuwa wachache walio chaguliwa akiwapo Danieli pamoja na vijana watatu marafiki zake, ambao walitwaliwa hadi utumwani. Nebukadreza mfalme wa Babeli yamkini alikuwa ameitoa amri kwamba, *'Nataka, uwalete baadhi ya wana wa Israeli, wa uzao wa kifalme, na wa uzao wa kiungwana; na vijana wasio na mawaa, wazuri wa uso, wajuzi wa hekima, werefu kwa sababu ya maarifa yao, wenye kufahamu elimu, wataoaweza kusimama katika jumba la mfalme; tena uwafundishe elimu ya Wakaldayo, na lugha yao.'* Mungu alikuwa akitumia amri ya maagizo yake mfalme wa kimataifa na mtu ili kuiweka huduma yake huko Babeli kwa ajili ya watu wake. Hii ni kwa sababu wakati mateka watakapokuwa wamehamishwa hadi huko Babeli, wangekuwa na ushawishi fulani katika makao yake Nebukadreza.

**Mifano Na Onyo**

Sura kumi na mbili za kitabu cha Danieli zimegawanywa katika sehemu mbili sawa. Sura za kwanza sita ni maelezo kuhusu historia. Sura ya saba hadi ya kumi na mbili ni ufunuo wa unabii. Kina cha sehemu zote za maelezo ya kihistoria katika Biblia na kile kinachopatikana

katika sura ya **1-6** ni msitari katika Agano Jipya, unaosema, *‘Basi mambo haya yaliwapata wao kwa jinsi ya mifano, yakaandikwa ili kutuonya sisi, tuliofikiliwa na miisho ya zamani* **(1 Wakorintho 10:11).’**

Katika Agano la Kale, unaweza kuona maisha ya kiroho ya watu wa Mungu yalikuwa ni kupanda na kushuka. Hata hivyo, haya si kweli kwa Yusufu na Danieli. Wao waliishi maisha yao katika mazingira maovu yenye desturi na mila za kisiasa za watawala wakuu duniani. Watu hao ni baadhi ya watu wakakatifu kabisa ambao utawapata katika Neno lake Mungu. Ingawa Yusufu aliishi kwenye mkono wa kulia wa Farao wa Misri, Danieli naye aliishi maisha yake katika desturi na tamaduni katili za utawala wa Babeli na Uajemi.

Daniel aliishi muda mrefu kuliko Nebukadreza na mwanawe, Belshaza. Alipata kuishi hadi kushuhudia milki ya Babeli ikianguka mikononi mwa utawala wa Uajemi. Yeye alinusurika na kuhudumu kama nabii kipindi chote cha miaka sabini ya utumwa huko Babeli. Alikuwa mkongwe na mdhaifu kuweza kurudi pamoja na mateka wale wengine hadi nchi yao, hata hivyo, alipata kuishi hadi kuona kurudi kwao kutoka nchi ya utumwa.

Ulikuwa ni wajibu wake Danieli kuwaonyesha watu wa Yuda jinsi ya kustahimili utumwani, wajibu ambao ulianza wakati ambapo alikuwa kijana wa miaka kumi na minne. Danieli alistahimili huko utumwani vyema kiasi kuwa alikuwa mfano kwa watu wa Yuda - na hata sisi siku ya leo.

**Azimio La Danieli**

Mtume Paulo aliandika: *‘Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu* ***(Warumi 12:2).’*** *Msitari huu umefafanuliwa zaidi hivi: ‘Usiruhusu ulimwengu kukubana katika mfumo wake bali mruhusu Mungu aiunde nia yako kutoka ndani.’* Hii ilikuwa ni himizo kwa waaminifu katika Agano Jipya, lakini kweli ya kanuni yake pia ilitumika wakati Danieli alipowasili huko Babeli.

Haikumchukua Danieli muda mrefu kutambua kulikuwa na msukumo kwake apate kufananishwa na desturi na mila za huko Babeli. Yeye alikuwa amechaguliwa na kulazimishwa katika chuo kikuu na kufundishwa na watu wenye maarifa wake Nebukadreza ili siku moja apate kuwa kiongozi mwema wa Babeli kwa niaba yao. Jambo la kwanza Danieli aliyokumbana nayo ilikuwa ni posho la vyakula vya kifalme vya huko Babeli. Yamkini chakula kile kilikuwa nyama ya nguruwe pamoja na vyakula vingine vingi vilivyokuwa najisi kwa kijana wa asili ya Kiyahudi kula. Tunasoma, *‘Lakini Danieli aliazimu moyoni mwake ya kuwa hatajitia unajisi kwa chakula cha mfalme, wala kwa divai aliyokunywa; basi akamwomba yule mkuu wa matowashi ampe ruhusa asijitie unajisi* **(Danieli 1:8)**.’

Jina la Danieli linamaanisha, ‘Mungu ndiye hakimu wangu.’ Danieli alienenda mbele za Mungu, akimwuliza Aihukumu kila hatua yake. Marafiki zake wale watatu pia walikuwa na majina yenye maana kuu ya kiroho. Mishaeli maana yake ilikuwa, ‘Ni nani aliye kama Mungu?’ Hanania nalo lilimaanisha ‘Yehova ndiye aliyejaliwa,’ na Azaria inamaanisha ‘Amesaidiwa na Yehova.’

Jambo la kwanza ambalo watu wa Babeli walifanya lilikuwa kubadilisha majina ya hawa vijana wa Kiebrania. Jina la Danieli lilibadilishwa na kuwa Belteshaza, ambalo lilimaanisha, ‘Bel yalinde maisha yake.’ Huyu Bel alikuwa mungu wa Babeli. Hawa Wababeli walikuwa wakijaribu kumfanya Danieli kuamini kwamba yeye angelikuwa chini ya ulinzi wa huyu mungu wa kimataifa. Jina la Mishaeli lilibadilishwa na kuwa Meshaki, mbalo ni Maduki katika Babeli. Maduki pia alikuwa ni mungu wa Babeli. Jina lake Hanania lilibadilishwa na kuwa Abednego, ambalo lilimaanisha ‘mtumishi wa mungu wa Babeli wa hekima **(Danieli 1:7).’**

Nebukadreza alikuwa akiwaambia hawa vijana wanne, ‘sisi tutawafanya ninyi kuwa Wababeli.’ Lakini Danieli pamoja na hawa vijana waliazimia kinyume chake Nebukadreza

pamoja na enzi yote na kuwaambia hivi, *'ninyi hamtatufanya kuwa Wababeli, bali sisi tutawafanya ninyi kuwa waaminifu!'*

Sura ya nne ya Danieli inatuambia Nebukadreza, mwenye maarifa ambaye aliileta pamoja enzi ya Babeli, alikiri imani katika Mungu. Hii ni moja wapo ya sura yenye kuvutia sana katika Biblia. Ni jambo gani ambalo lilimfanya Nebukadreza kuikiri imani? Haya yote yalianza wakati Danieli alikataa kujitia unajisi kwa posho la chakula cha Babeli.

**Utafsiri Wa Ndoto**

Hapo mapema katika utumwa, Danieli pamoja na marafiki zake walikumbana na pingamizi lingine. Nebukadneza alikuwa na ndoto, ambalo lilimfedhehesha sana. Aliwaita watu wake wote wenye maarifa na kuwaambia, 'Niambieni mimi ndoto ile niliyoota halafu mniambie maana yake.'

labda Jinsi unavyodhania, hii ilikuwa shida kuu kwa wenye maarifa huko Babeli. Kwa hakika, sio kazi kuu na ngumu kutafsiri ndoto, lakini mtu anawezaje kufahamu kwamba tafsiri yake ndio sahihi? Hili ndilo Nebukadreza alilokuwa akifikiria. Wakati Nebukadreza alipotia changa moto hii mbele ya hawa wenye maarifa, walihofia moyoni na kukata tamaa hata kuwaja na hamaki. Wakati kiongozi anapokuuliza kulitenda jambo fulani, basi huna budi kutenda lile wanalotaka au sivyo utajipata kwenye taabu na shida kubwa.

Wao walimwambia mfalme, *'Hapana mtu duniani awezaye kulionyesha neno hili la mfalme kwa maana hapana mfalme, wala bwana, wala liwali, aliyetaka neno kama hili kwa mganga, wala kwa mchawi, wala kwa Mkaldayo. Ni neno la ajabu, hili analolitaka mfalme, wala hapana mwingine awezaye kumwonyesha mfalme neno hilo, ila miungu, wasio na kikao pamoja na wenye mwili* **(Danieli 2:10-11)**.' Jibu hili lilimkasirisha Nebukadreza kiasi kwamba alitoa amri wenye maarifa wote wapate kuuawa. Hii ilikuwa ni pamoja na Danieli na marafiki zake kwa kuwa wao walikuwa wanafunzi wa hawa wenye maarifa.

Wakati mwuaji alipowasili ili kuwaua, Danieli alizungumza kwa busara na hadhari naye. Yeye aliuliza, '*Bona amri hii ya mfalme ina ukali mwingi namna hii? Naye yule mwuajia kwa jina Arioko, akida wa walinzi wa mfalme akajibu, 'Mfalme na watu wake wenye hekima walikuwa hawakubaliani. Wakuu wenye hekima walisema kwamba miungu hawaishi na wanadamu, na hivyo basi hawawezi kumwambia mfalme yale aliyoyaota.'*

Tafsiri nyepesi kwa muhtasari lake Danieli linaweza kuwa: 'Ee, bali hapo ndipo sisi tumekosea, kwa kuwa Mungu aishi ndani ya watu.' Naye Danieli akaingia, akamwomba mfalme na kumwuliza mfalme ampe muda, kisha yeye atamwonyesha mfalme tafsiri yake. Danieli baadaye akawaambia marafiki zake kile alichokuwa ametenda nao wakaanza kumwombea. Na katika njozi ya usiku, Mungu kwa njia isiyo ya kawaida akamfunulia siri hiyo ya ndoto yake Nebukadreza - pamoja na tafsiri yake.

Danieli alipata fursa yake kuwa na Nebukadreza, na majadiliano yao yalikuwa hivi: *'je! Waweza kunijulisha ile ndoto niliyoiona, na tafsiri yake'*. Danieli akamjibu mbele ya mfalme akasema, *'ile siri aliyoiuliza mfalme, wenye hekima hawawezi kumfunulia mfalme; wala wachawi, wala waganga, wana wajinamu; lakini yuko Mungu mbinguni afunuaye siri, naye amemjulisha mfalme Nebukadreza mambo yatakayokuwa siku za mwisho.'* Wakati Danieli alipomwambia Nebukadreza kile alichokuwa ameona katika ndoto pamoja na tafsiri yake, yule mfalme alianguka kifudifudi, akamsujudia

Danieli akatoa amri wamtolee sadaka na uvumba. Tangu siku hiyo mfalme alikuwa akimwita Danieli kama '*Mtu ambaye Roho wa Mungu akaa ndani yake* **(Sura 2).**'

Tafsiri ya Danieli ya ndoto yake mfalme ni moja wapo ya miujiza mitano ambayo imenakiliwa katika kitabu cha Danieli ambayo inadhihirisha kweli kuna kitu kisicho cha kawaida. Miujiza mingine minne ni: Kuokolewa kwa marafiki wake Danieli kutoka ndani ya tanuru yenye moto (sura ya tatu), Ungamo la imani lake Nebukadneza (sura ya nne), Maandiko juu ya ukuta (sura ya tano), Na kuokolewa kwa Danieli kutoka ndani ya tundu la simba (sura ya sita).

Kupitia miujiza hii, Danieli pamoja na marafiki zake walidhihirisha aina ya imani ambayo inaweza kustahimili nyakati ngumu. Wao walikuwa na imani ambayo iliamini katika uwezo usio wa kawaida wake Mungu, kikamilifu. Wao waliamini katika uwezo wa maombi, kikamilifu na pia katika kusudi lake Mungu aliyewafanya kuwepo Babeli.

Je! Umewahi kuwa na pingamizi katika maisha yako ambazo haungeweza kuziepuka, au kukwepa au hata kuvumilia pamoja na kukumbana na yale yasiyowezekana? Pingamizi zilizokumbana na Danieli pamoja na marafiki zake huko Babeli zilikuwa haziepukiki, hawangeweza kuzikwepa wala kuzivumilia. Watuonyesha jinsi ya kuishi katika pingamizi za aina ile, na je! Unafahamu kwamba wao waliishi na kukambili pingamizi zao huko Babeli.

Unapotafakari kuhusu miujiza hii katika kitabu cha Danieli, hebu jiulize maswali haya: je! Wewe unaamini katika nguvu za Mungu zisizo za kawaida? Je! Wewe unaamini katika uwezo usio wa kawaida katika maombi. Na je! Wewe unaamini katika Uungu wake Mungu pamoja na makusudio yake katika kukuweka mahali ulipo kwa ajili ya utukufu Wake? Je! Wewe unaamini mambo hayo kikamilifu?

## SURA YA KUMI NA MOJA

## 'Utukufu Uliokuwa Babeli'

Ingawa somo hili sio la wasomi, ila ni ukaguzi wa Biblia yote, kuna mitazamo ya kihistoria ambayo ni lazima uipokee na kufahamu ujumbe wa kitabu cha Danieli. Biblia mara nyingi hutumia utawala wa wafalme au Kaisari ili kuiweka tarehe ya matukio ya yake, kama ilivyo mistari ya kufungua kuhusu hadithi ya sikukuu ya kuzaliwa kwake Yesu Kristo -Krisimasi - iliopo katika sura ya pili ya Injli yake Luka.

Katika matukio yalionakiliwa katika sura nne za kwanza katika kitabu cha Danieli, Nebukadreza alikuwa ndiye mfalme wa enzi ya ulimwengu ya Babeli. Katika sura ya tano tunaelezwa kwamba mwanawe Nebukadreza, Belshaza ndiye mfalme. Na katika mistari ya kumalizia sura ile ya tano, pamoja na mistari ya kwanza ya sura ya sita ya Danieli, tunasoma kwamba Uajemi wamevamia na kuteka Babeli na Dario wa Mede ndiye mfalme. Kwa njia hii, Tunaelezwa kuwa sura sita za kwanza za Danieli zinajumuisha miaka sabini ya historia ya Babeli.

Matukio ya kihistoria ambayo yamenakiliwa katika nakala ya Biblia hujumuisha mataifa kama, Misri, Ashuru, Babeli, Uajemi, Uyunani na Roma. Katika kitabu cha Danieli, tunaona falme zikifuatana moja kwa nyingine - Ufalme wa Babeli ambao ulidumu kwa miaka sabini, na milki na utawala wa Uajemi wenye mikoa 127 ya Uajemi na Mede ambao pia ni sehemu ya kihistoria iliyopo katika kitabu cha Esta. Katika unabii mmoja uliopo katika Danieli, yeye anagusia baadhi ya falme hizi za dunia: Babeli, Uajemi, Uyunani na Roma.

Utafaidika kwa kuifahamu historia iliomo katika kitabu cha Danieli, pamoja na kuelewa sherehe na tamasha ya utukufu wake mfalme Nebukadreza, ikiwa unaweza kujifunza kitu kutoka mji wa Babeli. Hebu soma maelezo haya ya mji huo ambayo yaliandikwa na msomi mmoja wa historia ya Agano la Kale: *'Mji huu ulikuwa na wenyeji zaidi ya milioni mbili pamoja na mabustani yaliyokuwa yakining'inia huko Babeli ambayo yalikuwa mojawapo ya maajabu ya ulimwengu wa kale. Wasomi wa historia wanatueleza kwamba kuta zake zilizouzunguka mji ule zilikuwa za urefu wa maili mia moja na upana ya maili ishirini na tano kila upande. Na urefu wa kuta hizo ulikuwa yamkini mita mia moja kwenda juu na upana wake mita thelathini. Na kwenda chini ya ardhi kimo chake kilikuwa takribani mita kumi na tatu chini ya ardhi hivi kwamba hata maadui hawangeweza kupenya chini yake. Kulikuwepo na nafasi ya mita mia nne kuzizungukia kuta zile na ambapo hapakuwa na cho chote chenye kuzuia. Kuta zililindwa kote kwa mifereji au mitaro mipana yenye maji mengi. Kulikuwepo na vinara mia mbili hamsini vya walinzi kote juu ya kuta zile.*

*'Mji ule ulikuwa umegawanywa katikati kuwili na mto Frati. Na pande zote mbili za ufuo wake zililindwa na kuta za matofali na ambazo zilikuwa na malango yamkini ishirini na tano yaliyounganisha njia kwa mashua za feri. Kulikuwepo na daraja moja lililojengwa juu ya nguzo ambalo lilikuwa lenye urefu wa kilomita moja na mita kumi na moja urefu wake pamoja na daraja zilizoondolewa nyakati za usiku. Kulikuwepo na njia iliyopita chini ya mto ule, yenye upana wa mita saba pande zake na mita nne katika urefu wake wa juu. Na katika nyakati hizo za zamani, ule mji haungeweza kutekwa.'*

Katika siku zake Danieli, Babeli haukuwa tu mji wenye sifa kuu ulimwenguni, bali pia ndiyo uliyotawala na enzi yenye uwezo mkuu iliyoweza kuwepo wakati ule. Hata hivyo, ufalme huo uliweza kudumu kwa miaka sabini. Danieli alikuwa pale wakati wa kuinuka na kuanguka kwa ufalme huo. Yeye alikuwa rafiki na mshauri wake mfalme. Nebukadreza alikuwa mtu mwenye akili nyingi na mtawala mkuu ambaye aliujenga ufalme wa Babeli. Yeye aliutawala ufalme huo kwa miaka arubaini na mitano kati ya miaka yake sabini ya kudumu kwa ufalme ule.

Uwezo na mamlaka yake Nebukadreza yalikuwa bila upinzani. Na katika sura ya tano ya Danieli, tunasoma haya, *'aliyetaka mfalme kumwua alimwua; na aliyetaka kumwacha hai, alimwacha hai; aliyetaka kumtukuza, alimtukuza; na aliyetaka kumshusha, alimshusha (19).'* Ni vigumu sana kwa watu nyakati hizi kuelewa uwezo huu usio na kipimo wa kiongozi wa kimla kama huyu Nebukadreza. Unapopata habari za kihistoria kumhusu huyu kiongozi, unaweza kutambua kwamba ni muijiza mkuu unaoelezwa wakati kunakiliwa kwa ungamo lake la imani kwa Mungu wake Danieli.

Utambulizi wa kimuijiza wa ndoto yake mfalme Nebukadreza kutoka kwa Danieli, pamoja na tafsiri ya ndoto ile (sura ya 2), kulimshawishi sana kiongozi huyu wa ulimwengu wa siku zile. Katika ndoto ile, Nebukadreza aliona sanamu ya mtu. Kichwa chake kilikuwa cha dhahabu safi, kifua chake na mikono yake ni ya fedha; tumbo lake na viuno vyake ni vya shaba; miguu yake ni ya chuma na nyayo za miguu yake nusu ni chuma na nusu ni udongo.

Tafsiri ya Danieli ilikuwa kwamba kuna falme kuu nne za ulimwengu. Danieli alipo itafsiri ile ndoto yake Nebukadreza, alisema hivi, *'Wewe, ndiwe kichwa kile cha dhahabu kwa kuwa hadi*

*wakati huu wewe ndiwe mwenye ukuu, uwezo na nguvu, na utukufu ulimwenguni, lakini uwezo wako hautadumu muda mrefu. Baada ya zamani zako utainuka ufalme mwingine wa mdogo kuliko wewe; na ufalme mwingine wa tatu wa shaba utakaoitawala dunia yote. Ufalme wa nne utakuwa na nguvu mfano wa chuma; kwa maana chuma huvunja vitu vyote na kuvishinda; na kama chuma kisetavyo vitu hivi vyote, ndivyo utakavyovunja-vunja na kuseta. Mwishowe, ufalme ambao ni picha iliyomo katika nyayo za miguu ya chuma ni ufalme wa Warumi.'* Vile vidole kumi vyawakilisha maeneo kumi ya utawala wa Kirumi.

Yamkini, Nebukadreza alijawa na kiburi wakati aliposikia kwamba yeye ndiye 'kichwa cha dhahabu.' Na hivyo akaijenga sanamu ya dhahabu na kumfanya kila mtu kuiangukia chini na kuiabudu. Yeye alikuwa yu mbali sana na wokovu wakati huu! Bali kama vile tutakavyoona, ushuhuda wake Danieli na marafiki zake ulikuwa na ushawishi mkuu na uweza wa kuyabadilisha maisha yake Nebukadreza na ulimwongoza hadi katika ungamo la imani kwake Mungu wa kweli anayeishi.

**Nebukadreza Atubu**

Katika ndoto yake Nebukadreza, jiwe lilikatwa kutoka upande mmoja wa mlima, lakini sio kwa mikono yake mwanadamu. Jiwe hili lisilo la kawaida lilianguka juu ya miguu ya sanamu kuu yake Nebukadreza, katika miguu ambayo ilikuwa ya chuma pamoja na udongo. Tukio hili liliifanya sanamu ile kuanguka chini na kuvunjika vipande-vipande na kupasuka kama makapi katika kisagio. Tafsiri yake Danieli aliyompa Nebukadneza ilikuwa kwamba hizi falme zote, ambazo zilikuwa katika mfano wa dhahabu, fedha, shaba na chuma zitachukuliwa mateka siku moja na ufalme usio wa kawaida, ufalme wake Mungu.

Hatuna ufahamu wo wote kuhusu jinsi Mungu aliyatumia maisha na maneno yake Danieli ili kumfikia Nebukadreza, ila kwa njia ya muujiza, sura ya nne ya Danieli inasema hivi: *'Ni furaha yangu kukueleza kuhusu ishara za muijiza na maajabu ambayo Mungu aliye juu amenitendea. Jinsi gani ishara zake zilivyo kuu! Ufalme wake ni wa milele; utawala wa milki yake wadumu kutoka kizazi kimoja hadi kingine* **(2-3).**'

Katika sura hii ya ajabu ya Maandiko, Nebukadreza anatoa ndoto nyingine aliyomjia. Katika ndoto hii, yeye aliuona mti uliokuwa mrefu mno. Matawi yake yalijawa na matunda mengi sana hivi kwamba yangemtosha kila mmoja ulimwenguni. Halafu mmoja wa malaika wa Mungu akashuka chini kutoka mbinguni na kuipaza sauti yake akasema, '*Ukateni mti huu, yafyekeni matawi yake, yapukusieni majani yake, na kuyatawanya matunda yake, wanyama na waondoke hapo chini yake, na ndege katika matawi yake. Walakini kiacheni kisiki cha shina lake katika ardhi, pamoja na pingu ya chuma na shaba, katika majani mororo ya kondeni* **(Danieli 4:14-15)**.'

Yule malaika aliendelea kusema, *'Kikapate maji kwa umande wa mbinguni, na sehemu yake iwe pamoja na wanyama katika majani ya nchi; moyo wake ubadilike, usiwe moyo wa binadamu, na apewe moyo wa mnyama; nyakati saba zikapite juu yake* **(15-16).'** Yule malaika alisema kwamba kusudi la agizo lile ilikuwa kwamba ulimwengu upate kufahamu *'Aliye juu ndiye anayemiliki katika ufalme wa wanadamu, naye humpa yeye amtakaye, awaye yote.'*

Mfalme anatueleza pia alimweleza huyu Danieli ndoto hii yake. Wakati yule nabii aliposikia ile ndoto, alikaa pale akiwa ameduwaa na huku akiwa kimya kwa karibu muda wa saa mmoja, kwa mshangao wa tafsiri ile. Mwishowe akasema, *'Bwana wangu, ndoto hii iwapate wao wakuchukia, na tafsiri yake iwapate maadui zako* **(19).'**

Baada ya mfalme kumsihi Danieli kumpa tafsiri ya ndoto ile, Danieli alisema haya, *'Tafsiri yake ni hii, Ee Mfalme, nayo ni amri yake aliye juu, iliyomjia bwana wangu, mfalme, ya kuwa utafukuzwa mbali na wanadamu, na makao yako yatakuwa pamoja na wanyama wa kondeni. Nawe utalazimizhwa kula majani kama ng'ombe, nawe utatiwa maji ya umande wa mbinguni, na nyakati saba zitapita juu yako; hata utakapojua ya kuwa Aliye juu ndiye anayemiliki katika ufalme wa wanadamu, naye humpa yeye amtakaye, awaye yote* **(25)**.'

Hata hivyo, Danieli aliendela kusema kwamba Mungu ataurudisha ufalme ule kwake wakati yeye atakapotambua ukuu Wake. Naye Danieli akamsihi, *'Ee mfalme, shauri langu lipate kibali kwako; ukaache dhambi zako kwa kutenda haki, ukaache maovu yako kwa kuwahurumia maskini; huenda ukapata kuzidishiwa siku zako za kukaa raha* **(27).**'

Danieli anaandika mistari inayoeleza kutimizwa kwa tafsiri ya ndoto ile. Na baada ya tukio hili bovu, Nebukadreza anarudia kuandika kwa kukiri imani yake na kumsifu Mungu anayeishi wake Danieli. Aliyainua macho yake mbinguni na kumsifu, na kumheshimu pamoja na kumtukuza Mungu Mkuu!

Waweza kuona kwamba Mungu alikuwa na kusudi kwa kumfanya Nebukadreza kupitia hali hii mbovu: ili kujifunza kwamba Mungu Mkuu anatawala watu ulimwenguni wote. Ilimbidi huyu Nebukadreza kuishi kama mnyama nyakati saba hadi atakapojifunza kile ambacho Mungu alimtaka kujifunza. Inaonekana kwamba huyu Nebukadreza alikuwa mwenye moyo mgumu hivi kwamba ilimchukua Mungu miaka saba kumfanya aliyekuwa mtawala wa ulimwengu kulegeza kichwa chake.

Yawezekana kuwa kuna wakati sisi hupitia katika hali mbaya kwa kuwa Mungu anajaribu kutuonyesha kwamba Yeye ana haki yote katika kutawala ulimwengu huu pamoja na maisha yetu? Wakati haya yanapotukia, je! Inakuchukua muda gani kabla hujamwambia Mungu, *'Bwana wangu na Mungu wangu! Wewe ndiwe kiongozi. Wewe ndiwe mfalme mkuu na una uweza wote katika maisha yangu?'*

# SURA YA KUMI NA MBILI

## 'Maono Na Ufunuo Wa Danieli'

Kwa kuwa sura za mwanzo sita za Danieli ni historia, ni nyepesi mno kuzielewa au kuzifahamu. Sura sita za mwisho, jinsi ilivyo katika kitabu cha Ufunuo pamoja na utabiri wa Ezekieli na Zakaria, ni ngumu mno kuzifahamu. Tafsiri yake Danieli kwa ndoto ya Nebukadreza ya kwanza, katika Danieli sura ya 2, inatupatia mfumo ambao unatupatia mwongozo wakati tunapojaribu kutafsiri maono na ufunuo katika Kitabu cha Danieli. Ni katika huduma ya mafundisho ya Roho Mtakatifu, tunaweza kufahamu maono na Ufunuo wa unabii wa kazi kubwa ya Mungu katika ulimwengu wetu.

Kuna baadhi ya hatua ambazo tunahitaji kuzichukuwa ili kujaribu kufahamu maono na ufunuo katika Danieli. Kwanza, tazama ishara zilizo katika maono. Kwa mfano, katika maono ya kwanza ambayo ni magumu yake Danieli, ambayo yame nakiliwa katika sura ya saba, ishara za maono hayo ni sawa na zile zilio katika ndoto ya Nebukadreza.

Pepo kuu nne zilianza kuvuma na kuchafua bahari kuu, kisha wanyama wanne waibuka. Mnyama wa nne alikuwa mbaya na katili hivyo basi aliwagandamiza wanyama wale wengine,

lakini kabla ya kuwagandamiza, pembe kumi zilitokea. Pembe ile ndogo ilikuwa na macho na kinywa kikubwa, na ilizungumza mambo makuu na makubwa.

Pili, tazama tendo na ushirikiano kati ya ishara hizo. Tilia maanani matendo na ushirikiano katika ishara. Pia tilia maanani tafsiri ambayo imo katika fungu lile la Maandiko yale, ambayo ni tafsiri iliyovuviwa ya kifungu kile. Baada ya kutenda hivyo, kwa njia ya maombi mwulize Roho Mtakatifu kukuonyesha maana yake. Jiulize mwenyewe, *'Maandiko haya yanasema nini, maana yake ni nini, na maana yake kwao ni ipi, kisha maana yake kwangu ni ipi?'*

Tafsiri iliyovuviwa ya ndoto ya Danieli iliopo katika sura ya saba inatuambia kwa mara nyingi sisi huzitazama falme kuu nne. *'Wanyama wale wanne wakuu ni falme nne ambazo zitaibuka kutoka ulimwenguni. Lakini watakatifu wake Mungu aliye juu wataupokea ufalme na kuumiliki milele - naam, milele hata milele* **(17-18)**.' Ufalme mwingine wa nne utatokea katika ulimwengu na kuagamiza kabisa. Zile pembe kumi ni wafalme kumi ambao watatoka katika ufalme ule. *'Na baadaye mfalme mwingine ataibuka, tofauti kabisa nao wale wa kwanza; naye atawatiisha wale wafalme watatu. Yeye atazungumza kinyume chake Mungu aliye juu na kuwatesa watakatifu wake na hata kujaribu kuzibadilisha nyakati na sheria. Nao watakatifu watadhoofishwa chini yake kwa wakati, na nyakati mbili na nusu wakati* **24-25).**'

Wakati wo wote ule pembe inapotajwa katika Biblia, hiyo huwakilisha mamlaka au uwezo, kama vile pembe zilizomo juu ya wanyama ambazo hutumiwa kuwapiga vita wanyama wale wengine. Hizi pembe kumi na ile ndogo pia zinawakilisha mamlaka au falme. Watu wengi hutafisiri huu ufalme wa nne kama enzi iliyofufuliwa ya Kirumi. Katika maono ya Nebukadreza, ile miguu ya chuma - falme ya nne - iliwakilisha Ufalme ya Kirumi. Wengine wanaamini kwamba maono yale pia yanawakilisha ufalme wa Kirumi uliofufuliwa lakini hapo baadaye. Hali wengine wanasema sivyo, falme hii ya nne ni yenye ukatili mkuu kuliko falme nyingine. Ni picha ya ufalme wake Mungu na kwa njia ya unabii inawakilisha na kudhihirisha hukumu kali yake Mungu.

Katika maoni yangu mwenyewe, hatuwezi kwa hakika kuthibitisha tafsiri hizi za Danieli. Haijalishi kana kwamba tunafahamu kwa uhakika kuhusu utimilifu wote, na ni lazima tukumbuke kweli hii kubwa kutoka kwa unabii huu uliopo katika sura ya saba ya Danieli: ikiwa wewe ni mmoja wa watu wake Mungu, basi u sehemu ya ufalme ambao utakuwa na ushindi mkuu. Maono haya yote yanamalizikia kwa tumaini kuu. Maono haya yanaonyesha picha kuhusu falme yake Mungu ikupata ushindi juu ya falme zingine zote na kufanyika ufalme wa milele.

**Maono Ya Majuma Sabini**

Maono ya Danieli yenye kufahamika sana au ufunuo wa unabii unafahamika kama, 'maono ya majuma sabini.' Danieli anatuambia alipokuwa akisoma unabii wake Yeremia, alitambua ulikuwa ndio wakati wa watu wake Mungu kurudi kutoka nchini Babeli hadi nchi yao. Isaya pamoja na Yeremia walikuwa wametabiri kwamba baada ya watu wa Yuda kuwa utumwani huko Babeli kwa miaka sabini, wao wangelirudi katika nchi yao wenyewe. Wakati Danieli atuambia hapo mwishoni mwa sura ile ya tano na mwanzoni wa sura ya sita kwamba yeye

alikuwa chini ya utawala wa Dario Mmedi, alikuwa akielezea mwisho wa miaka sabini huko utumwani.

Danieli akifanya maombi yake makuu katika sura ya tisa, kwa hakika, akiwa na hamu kuwa kwa kweli miaka ile sabini ilikuwa imewadia. Huku Danieli akizidi kuomba kulihusu jambo hili, akiziungama dhambi zake na zile za watu wake. Danieli alikuwa mmoja wa watu wenye utakatifu wa kimaisha na tabia katika Biblia. Hivyo, alijitambulisha mwenyewe na dhambi za watu wake kwa kusema mambo haya, 'Dhambi zetu' na 'sisi tumezitenda dhambi,' mara thelathini na mbili katika maombi yale.

Danieli alimwomba Mungu msamaha. Hakika, alisema, 'Mungu wewe hauko tu tayari kutusamehe sisi, bali pia wewe uko tayari kuturudi.' Katika maombi yake, kwa hakika amejawa na msisimuko kwamba Mungu alikuwa awasamehe na kuwarudisha kama watu wake.

Danieli alipokuwa akiomba, malaika alimtokea na kusema, *'Mwanzo wa maombi yako ilitolewa amri, nami nimekuja kukupasha habari habari.........***(Danieli 9:23).'** Haya yalikuwa majibu ya Mungu kwa maombi ya Danieli, moja wapo ya unabii sahihi kabisa wa Kimasihi unaopatikana mahali po pote katika Biblia. Maono yalikuwa kwamba: *Wiki sabini za miaka ziliangizwa kuwahusu watu wako pamoja na mji wako mtakatifu. Haya ndiyo makusudio ya majuma haya sabini ambayo yaliagizwa - kumaliza uovu, kuiondolea mbali dhambi, kufanya upatanisho kwa ajili ya dhambi, na kuileta ndani haki, na kuitia muhuri maono yale pamoja na unabii, na kupaka mafuta Mahali palipo Patakatifu.'*

Pamoja na habari njema kuwa kurudi kwao kulikaribia, kuna ujumbe kuhusu kuja kwa mara ya kwanza kwake Masihi, Yesu Kristo. Tafsiri ya unabii huu usio-wa kawaida unahusisha hesabu nyepesi. Mungu anamwambia Danieli, jinsi utumwa ulivyokuwa miaka sabini, kipindi cha mjio wa kwanza au kuja kwa Masihi Yesu Kristo. Tafsiri ya miaka hii inahusu baadhi ya hesabu rahisi. Mungu anamweleza Danieli kuwa wakati utumwa unapodumu kwa kipindi cha miaka sabini, muda ulio kati ya utumwa na mjio wa Masihi ungekuwa saba mara sabini, au miaka mia nne na tisini. Miaka hii ingegawanywa katika majuma ya miaka (nyakati saba za miaka), na upande mwingine, majuma haya sabini ya miaka yangeligawanywa hivi: majuma saba, majuma sitini na mawili, na juma moja. Na katikati wa juma mmoja, Yule Mtiwa mafuta 'Atafutiliwa mbali,' au atauawa.

Unabii huu unawahitaji kuelezewa kutoka wakati mfalme Koreshi ilipotoa agizo kwamba watu wa Yuda wangeweza kurudi na kuijenga Yerusalemu. Kulikuwepo na makundi matatu tofauti yaliyorudi, lakini ile ya kuu ilikuwa mnamo mwaka wa 457 Kabla ya Kuzaliwa kwake Yesu Kristo. Ukichukua majuma yale sitini na mawili na kuyaongeza majuma saba, na kufanya mara saba, jumla ya hesabu ile ni miaka 483. Songa mbele katika historia miaka hiyo mingi tangu mwaka wa 457 kabla ya Kuzaliwa kwa Yesu Kristo na utafikia mwaka wa 26 baada ya Kuzaliwa Yesu Kristo, ambao wasomi wanatueleza kwamba huo ulikuwa ndio mwaka ambao Masihi

alianza huduma yake kwa jamii. Ilikuwa kuwe na juma la miaka, (au miaka saba), kufuatia hiyo, hapa katikati mwa juma lile la miaka Yule Mtakatifu angalikatiliwa mbali au kuondolewa. Wasomi wanaamini kwamba baada ya miaka mitatu na nusu tangu mwaka wa 26 Baada ya Kuzaliwa kwake Yesu Kristo, ndio wakati Yesu Kristo aliposulubiwa.

Ingawa wasomi wanatofautiana katika mambo madogo madogo, jambo moja ambalo ni dhahiri kabisa kuhusu unabii huu ni utabiri wa kiajabu sana hasa ukisiao wakati ule wa kuja kwake pamoja na kusulubishwa kwa Masihi na mwanzo wa utawala wa milki yake, ambao hautakuwa na mwisho. Huu utakuwa ndio ufalme ambao ulitajwa kwa njia ya unabii katika ndoto/maono ya pili ya Nebukadreza, ambao Danieli alimtafsiria **(2:34,35,44,45).** Ufalme ule ulikuwa ume elezwa kama jiwe kubwa ambalo lilianguka juu ya miguu ya sanamu ile iliyowakilisha falme nne za ulimwengu na kuzivunja kama makapi.

Sehemu ya sanamu ambayo jiwe lile liliangukia ilikuwa ni sehemu iliyowakilisha enzi au milki ya Warumi. Hii kwa hakika, ilitabiri kwamba Yesu alianza ufalme wake nyakati za enzi na utawala wa Kirumi, na kwamba ufalme wa Mungu ulizinduliwa na Yesu, ambao kwa wakati huu umetamalaki kwa miaka mingi kuliko ule wa Kirumi kwa jumla ya miaka elfu mbili, na hautakuwa na mwisho.

**Matumizi Ya Kibinafsi Ya Unabii Huu**

Mojawapo ya tafsiri iliyo dhahiri pamoja na matumizi ya maono na unabii huu wa kimiujiza ni kwamba wale ambao ni sehemu ya Ufalme huu wa milele wana uzima wa milele kwa kuwa wao ni sehemu ya ufalme huo.

Ili kubadilisha msemo, ikiwa wewe ni mwaminifu, na ikiwa wewe ni mmoja wa watu wa Mungu, basi u askari jeshi katika jeshi ambalo litakwenda kushinda vita kati ya wema na uovu. Vita kati ya wema na uovu vimepiganwa kwa muda wa maelfu ya miaka katika sehemu nyingi ulimwenguni hata siku ya leo. Mazingira yake yanabadilika kila wakati; wema na uovu hujivika nyuso tofauti, lakini vita vile vimekuwa vikipiganwa tangu wakati Kaini alipomwua nduguye Habili.

**Raia Au Wenyeji Wa Mbinguni**

Mtume Paulo anaandika uenyeji wetu ni wa mbinguni nayo Maandiko yanatueleza kwamba watu wa imani ni wasafiri wanaopita dunia hii huku wakiutafuta mji wenye misingi yake iliyobuniwa ambaye Mjenzi wake ni Mungu. Watu wake Mungu wanaelezwa kama mto ambao unaenea kote katika ulimwengu huu hadi mji wake Mungu ambapo kutakuwa na furaha kuu wakati utakapowasili pale **(Waebrania 11:13-16; Zaburi 46:4,5).**

Kwa kuwa wewe ni mwenyeji wa Ufalme ule usio na mwisho, Je! Unashiriki katika ushindi ambao Yeye na Babake Mungu wana uhakika wa kuupata? Yesu Kristo ndiye Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana, na kiongozi ambaye hapo mwishowe atashinda nguvu za uovu zilio katika ulimwengu huu. Ikiwa sisi tu wanafunzi wake wa kweli, hakika tu askari wa jeshi Lake

la Kiroho. Yawezekana kwetu kushindwa mapigano mengine katika safari yetu, lakini tutashinda vita vikuu. Katika uzima wa milele, sisi tutaishi kwa ufahamu wa kweli hii: Kulingana na kiwango ambacho tulikuwa sehemu ya ushindi Wake ambao ilithibitisha dhamana ya uzima wetu wa milele.